# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MTAALA WA ELIMU YA MSINGI

# DARASA LA I – VII

© Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2015

Toleo la Kwanza, 2015
Toleo la Pili, 2016
Toleo la Tatu, 2019

ISBN: 978 - 9987 - 09 - 055 - 6

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam

| | |
|---|---|
| Simu: | +255 22 2773005/+255 22 277 1358 |
| Nukushi: | +255 22 2774420 |
| Baruapepe: | director.general@tie.go.tz |
| Tovuti: | www.tie.go.tz |

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2015). Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I-VII. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kufasili andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

# Yaliyomo


**Orodha ya majedwali** .......................................................................... vi
**Vifupisho** ........................................................................................ vii
**Ujumbe Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu** ...................................... viii
**Dibaji** ................................................................................................ ix
**Utangulizi** .......................................................................................... 1
1.1 Usuli ............................................................................................ 1
1.2 Muktadha wa Mtaala wa Elimu ya Msingi ........................ 2
**Mambo Yaliyozingatiwa katika Uandaaji wa Mtaala** ................. 3
2.1 Utangulizi ................................................................................ 3
2.2 Sheria ya Elimu Namba 25 ................................................ 3
2.3 Matamko ya Kisera ............................................................ 3
2.4 Matamko ya Kitaifa na Kimataifa ...................................... 4
2.5 Kiunzi cha Mtaala wa Taifa kwa Elimumsingi na Elimu Ualimu .................................................................................... 6
2.6 Mitazamo ya Mtaala ............................................................ 6
**Mchakato wa Uandaaji wa Mtaala** ................................................ 8
3.1 Utangulizi ................................................................................ 8
3.2 Hatua za Kuandaa Mtaala ................................................. 8
**Ushiriki wa Wadau wa Elimu katika Uandaaji wa Mtaala** ......... 10
4.1 Utangulizi ................................................................................ 10
4.2 Ushiriki wa Wazazi na Jamii ............................................. 10
4.3 Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi ................................ 10
**Malengo na Umahiri katika Mtaala wa Elimu ya Msingi** ............ 11
5.1 Utangulizi ................................................................................ 11
5.2 Malengo ya Elimu ya Msingi ............................................. 11
5.3 Umahiri katika Elimu ya Msingi ........................................ 12
5.4 Walengwa wa Mtaala ......................................................... 13
**Maeneo ya Umahiri katika Darasa la I-II** ..................................... 14
6.1 Utangulizi ................................................................................ 14
6.2 Umahiri katika Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ............. 14
6.3 Umahiri katika Stadi Wezeshi ............................................ 15
6.4 Muda wa Kufundisha na Idadi ya Vipindi Darasa la I-II ... 16

**Maeneo ya Kujifunza Darasa la III-VII** ........................................ 17
7.1 Utangulizi ........................................................................ 17
7.2 Maeneo Makuu ya Kujifunza ............................................ 17
7.3 Mgawanyiko wa Masomo .................................................. 19
7.4 Umahiri katika Masomo .................................................... 20
**Masuala Mtambuka** ........................................................................ 35
8.1 Utangulizi ........................................................................ 35
8.2 Uchopekaji wa Masuala Mtambuka katika Mtaala ............ 36
**Mgawanyo wa Muda wa Kufundishia Masomo kwa Darasa la III-VII** ............................................................................ 40
9.1 Utangulizi ........................................................................ 40
9.2 Mgawanyo wa Muda ......................................................... 40
**Kujifunza Somo la Elimu ya Dini** .................................................. 43
10.1 Utangulizi ........................................................................ 43
10.2 Siku za Kujifunza Somo la Elimu ya Dini ........................ 43
**Ufundishaji na Ujifunzaji** ................................................................ 44
11.1 Utangulizi ........................................................................ 44
11.2 Madarasa Jumuishi na Madarasa Maalum ......................... 44
11.3 Shughuli katika Mtaala wa Ziada ....................................... 49
**Rasilimali katika Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi** .... 52
12.1 Utangulizi ........................................................................ 52
12.2 Rasilimali Watu ................................................................. 52
12.3 Rasilimali Vitu ................................................................... 53
12.4 Rasilimali Muda ................................................................. 56
12.5 Rasilimali Fedha ................................................................ 56
**Upimaji wa Maendeleo ya Mwanafunzi** ........................................ 57
13.1 Utangulizi ........................................................................ 57
13.2 Upimaji wa Awali ............................................................... 57
13.3 Upimaji Gunduzi na Majaribio Chekeche.......................... 57
13.4 Upimaji Endelevu ............................................................... 58
13.5 Upimaji Tamati ................................................................... 58
13.6 Upimaji wa Kitaifa.............................................................. 59

**Usimamizi wa Mtaala** ........................................................................ 61
14.1 Utangulizi ............................................................................ 61
14.2 Majukumu ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ............... 61
14.3 Mafunzo Endelevu ya Mtaala kwa Watekelezaji ............... 61
14.4 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtaala wa Elimu ya Msingi ..... 62
**Ujifunzaji na Viwango vya Upimaji Darasa la III-VII** ................ 63
15.1 Utangulizi ............................................................................ 63
15.2 Vigezo na Viwango vya Kupima ........................................ 63
**Marejeleo** .......................................................................................... 72

# Orodha ya Majedwali

**Jedwali**


1. Umahiri Katika KKK Darasa la I ............................................ 14
2. Umahiri katika KKK Darasa la II ............................................ 15
3. Umahiri katika stadi wezeshi Darasa la I-II ............................. 15
4. Mgawanyo wa muda na vipindi kwa Darasa la I-II ................ 16
5. Mgawanyo wa masomo kwa Darasa la III-VII ........................ 19
6. Masomo ya kuchagua katika Mtaala wa Ziada ....................... 20
7. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Kiswahili ................... 20
8. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Kiingereza ................ 22
9. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Hisabati ...................... 23
10. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Sayansi na Teknolojia ......................................................................... 25
11. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Maarifa ya Jamii ........ 26
12. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Stadi za Kazi ............. 27
13. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Uraia na Maadili ........ 28
14. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Kifaransa .................. 31
15. Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Kiarabu ...................... 33
16. Mgawanyo wa masuala mtambuka kulingana na somo bebezi na darasa linalohusika ............................................................... 35
17. Umahiri katika masuala mtambuka kimadarasa ....................... 36
18. Muda na idadi ya vipindi kwa kila somo katika wiki .............. 41
19. Ufundishaji na Ujifunzaji katika madarasa jumuishi na madarasa maalum ......................................................................... 44
20. Umahiri katika shughuli za michezo na sanaa kwa Darasa la III – VII ..................................................................... 50
21. Vigezo na viwango vya kupima utendaji wa mwanafunzi wa Darasa la III-VII ......................................................................... 63
22a. Vigezo na viwango vya kupima utendaji wa mwanafunzi wa Darasa la III - VII katika Somo la Kiarabu ............................. 69
22b. Tafsiri ya maneno ya Kiarabu katika Jedwali Na 22a ............. 70
23. Vigezo na viwango vya kupima shughuli katika Mtaala wa Ziada ... 70

| | |
|---|---|
| KKK | Kusoma, Kuandika na Kuhesabu |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania |
| MMEM | Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |
| WyEMU | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| WyEU | Wizara ya Elimu na Utamaduni |

## Ujumbe Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu

Elimu ni mchakato unaotoa maarifa, ujuzi, maadili na stadi za maisha kwa walengwa. Mchakato huu una lengo la kumwandaa mwanafunzi kuweza kukabili mazingira yake na kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya jamii inayomzunguka na taifa kwa ujumla. Mojawapo ya malengo ya elimu nchini Tanzania ni kutoa elimu bora itakayowawezesha wahitimu kushiriki kikamilifu katika jitihada za serikali za kuwezesha uchumi wa nchi kukua na kufikia uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025. Hili ndilo lengo kuu ambalo mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I-VII unalenga kulifikia. Vilevile mtaala umelenga kumjengea mwanafunzi uzoefu mpana wa kujifunza na unasisitiza matumizi ya mbinu shirikishi za kufundishia na kujifunzia ambazo zinagusa mahitaji ya kila mwanafunzi. Msisitizo upo katika kumjenga mwanafunzi katika nyanja zote za kujifunza: kiroho, kimaadili, kiakili, kimwili na kijamii.

Mtaala huu umeandaliwa kwa viwango vinavyokidhi haja ya kujifunza kwa ufanisi ili kumjengea mwanafunzi umahiri katika Elimu ya Msingi. Kwa hiyo umezingatia matakwa ya Sheria ya Elimu na matamko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Ni matumaini yangu kwamba maudhui ya mtaala huu yatawaongoza watekelezaji kutumia fursa walizonazo kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri utakaomsaidia kuyamudu maisha yake katika jamii inayomzunguka. Ili kubaini kiwango cha mafanikio katika ujifunzaji, upimaji utafanyika kwa kuzingatia uwezo wa mwanafunzi kutenda na uwezo wake katika kujipima mwenyewe.

Ninatambua kwamba tunaishi katika jamii ambayo mahitaji yake yanabadilika siku hadi siku kutokana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia na kiuchumi. Hivyo, mtaala utaendelea kuboreshwa sambamba na mabadiliko yanayotokea kila baada ya kukamilika kwa mzunguko mmoja wa wahitimu yaani miaka saba. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa niaba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) iko tayari kupokea maoni ya kuboresha mtaala huu kutoka kwa walimu na wadau wengine wa elimu. Maoni yote yapelekwe kwa Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Elimu, Tanzania.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru wadau wa elimu kutoka taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali ambao kwa namna moja au nyingine wamefanikisha uandaaji wa Mtaala Elimu ya Msingi.

-----------------------------------

**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**


# Dibaji

Elimu bora ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. Mtaala wa Elimu ya Msingi umeandaliwa kwa kuzingatia kuwa elimu inayotolewa ni bora na inamwezesha mwanafunzi kujenga umahiri unaohitajika katika kukabili mabadiliko ya kijamii, kielimu na kiuchumi. Andiko hili la mtaala linafanua utoaji wa Elimu ya Msinsi Tanzania kwa kuzingatia Sheria ya Elimu na falsafa inayoongoza utoaji wa elimu hiyo. Andiko hili linaeleza malengo ya elimu, maeneo ya kujifunza na umahiri anaotarajiwa mwanafunzi kuupata katika kila eneo la kujifunza. Aidha, andiko linaelezea utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi nchini, mgawanyo wa muda wa kufundisha na kujifunza masomo, taratibu za ufundishaji na ujifunzaji na rasilimali katika utekelezaji wa mtaala huu. Vilevile, mtaala umetoa mwelekeo wa na namna upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi, namna mtaala utakavyosimamiwa na kufafanua ujifunzaji na viwango vya upimaji.

Mtaala huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka saba. Utekelezaji umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni katika kipindi cha miaka miwili ya mwanzo, yaani Darasa la I-II. Katika sehemu hii mtaala umejikita katika kumjengea mwanafunzi umahiri katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Sehemu hii imeandaliwa kwa kuzingatia kwamba miaka ya mwanzo ya kujifunza ni muhimu sana katika makuzi ya mtoto kiakili, kimwili na kijamii.

Sehemu ya pili ni Darasa la III-VII. Maudhui katika sehemu hii yameandaliwa katika mtindo wa kukuza umahiri katika masomo nane ambayo ni: Kiswahili, Kiingereza, Hisabati, Uraia na Maadili, Sayansi na Teknolojia, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi na masomo chaguzi ya lugha (Kifaransa na Kiarabu). Hata hivyo, katika sehemu hii umahiri wa KKK unaendelea kupewa msisitizo katika masomo. Hii ni kwa sababu KKK ni msingi muhimu katika kumwezesha mwanafunzi kujifunza masomo haya kwa ufanisi. Kazi kubwa ya mwalimu ni kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kujenga umahiri unaokusudiwa.

Mtaala huu umetafsiriwa katika miongozo mbalimbali itakayosaidia kufafanua namna ya kuutekeleza kama ilivyokusudiwa. Mwongozo mkuu katika utekelezaji wa kila umahiri unaokusudiwa ni muhtasari ambao utatumiwa na mwalimu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu hana budi kuupitia muhtasari kwa umakini ili aweze kuwa na mtazamo mpana kuhusu kile anachotakiwa kukifundisha. Ni matarajio yangu kuwa muhtasari utamwongoza mwalimu kufanya kazi yake kwa ufanisi. Ni muhimu pia kwa wadau wengine wa elimu kutumia mtaala huu katika kutekeleza na kufuatilia ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto kwa kuzingatia umahiri katika Darasa la I-II na masomo ya Darasa la III-VII.



.....................................

**Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa**
**Kaimu Kamishna wa Elimu**
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# Utangulizi

## 1.1 Usuli

Marekebisho ya Mtaala wa Elimu ya Msingi (2015) yamezingatia mahitaji ya Sheria ya Elimu ya mwaka 2002, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Sera ya Elimu 2014, Mpango wa Kisekta wa Maendeleo ya Elimu wa mwaka 1999 – 2009, na Dira ya Maendeleo ya Tanzania hadi mwaka 2025. Vilevile marekebisho yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) wa mwaka 2000 - 2006, Mpango wa Taifa wa Kuinua Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), na mapendekezo ya tafiti anuai za kielimu. Ikumbukwe kuwa Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 1997 uliweka msisitizo katika maudhui ya masomo. Uboreshaji wa mtaala huu ulifanyika mwaka 2005 na kuweka msisitizo katika umahiri. Pamoja na maboresho ya mwaka 2005, tafiti mbalimbali zimeonesha kuwa mtaala ulioboreshwa bado ulikuwa umejikita zaidi katika maudhui ya masomo kuliko umahiri.

Mwaka 2013 ulifanyika utafiti wa kitaifa juu ya utekelezaji wa mtaala wa mwaka 2005. Lengo la utafiti huo lilikuwa ni kupima uwezo wa wanafunzi wa Darasa la II katika stadi za KKK. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwepo kwa wanafunzi wenye matatizo katika stadi za msingi za KKK. Vilevile, matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa mtaala wa Darasa la I na la II ulikuwa umesheheni masomo mengi na kuwafanya walimu kufundisha maudhui ya masomo kuliko stadi za KKK. Kutokana na upungufu huo ilionekana kuwa ni muhimu kuandaa mtaala ambao utazingatia ufundishaji wa umahiri katika KKK kwa Darasa la I - II. Hivyo, mwaka 2015, Wizara ya Elimu ilianza kazi ya kuboresha Mtaala wa Elimu ya Msingi. Kazi hii ilifanyika kwa awamu tatu. Katika awamu ya kwanza mtaala uliboreshwa kwa kufuta masomo yote na kuweka mkazo katika kukuza umahiri katika KKK kwa Darasa la I-II.

Awamu ya pili ya uboreshaji wa mtaala wa mwaka 2016 ilihusisha mtaala wa Darasa la III-VI. Uboreshaji huo ilihusisha kuunganisha baadhi ya masomo. Kwa mfano, masomo ya Jiografia na Historia yaliunganishwa na kuwa Somo la Maarifa ya Jamii.

Awamu ya tatu ya uboreshaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi ilikuwa mwaka 2019. Kazi kubwa katika awamu hii ilikuwa kukamilisha uboreshaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi kwa kuaandaa mihtasari ya masomo ya Darasa la VII na kuunganisha mtaala kuanzia Darasa la I-VII. Maboresho hayo yameimarisha mwendelezo wenye mantiki kutoka Darasa la I-VII. Aidha, yamekidhi mahitaji ya kijamii, kisayansi na kiteknolojia kwa kuzingatia ufundishaji na ujifunzaji ambao unamwezesha mwanafunzi kujenga maana.

## 1.2 Muktadha wa Mtaala wa Elimu ya Msingi Darasa la I -VII

Mtaala huu umeandaliwa katika muktadha wa kuhakikisha utoaji wa elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya Mtanzania na yenye kutoa fursa sawa za kujifunza kwa wanafunzi wote. Mtaala umezingatia masuala mbalimbali ikiwemo stadi za Karne ya 21, kukua kwa Sayansi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na utandawazi. Unalenga kuhakikisha kuwa Elimu ya Msingi inayotolewa ni bora na wahitimu wake wanakuwa ni wazalendo, wanaojitegemea na wenye uwezo wa kuongea lugha zaidi ya moja. Aidha, Elimu ya Msingi inatarajiwa kutoa wahitimu wenye maarifa na stadi mbalimbali zitakazowawezesha kuchangia katika kuifikisha Tanzania katika uchumi wa viwanda. Mtaala pia unasisitiza utoaji wa elimu jumuishi, yaani elimu inayothamini na kuheshimu uwezo, mahitaji, jinsia na kutambua kwamba wanafunzi wote wanaweza kujifunza na kufanikiwa. Aidha mtaala huu unatarajiwa kukidhi matakwa ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kumwandaa mwanafunzi wa Tanzania kuishi katika ulimwengu wenye ushindani

Mtaala huu umegawanywa katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Darasa la I-II. Lengo kuu katika sehemu hii ni kujenga umahiri katika stadi za KKK. Sehemu ya pili inaanzia Darasa la III- VII. Lengo kuu katika sehemu hii ni kumwezesha mwanafunzi kujenga ujuzi katika stadi za KKK pamoja na ujuzi katika stadi nyingine za maisha kupitia masomo ya Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi, Kiswahili, Hesabu, Sayansi na Teknolojia, Uraia na Maadili, Kiingereza na masomo chaguzi ya lugha (Kifaransa na Kiarabu). Inatarajiwa kuwa mtaala huu utatekelezwa kwa ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

# Mambo Yaliyozingatiwa katika Uandaaji wa Mtaala

## 2.1 Utangulizi

Mtaala huu umezingatia kwamba Elimu ya Msingi itakuwa ni ya miaka saba ili kufikia umahiri uliokusudiwa. Mtaala umeandaliwa kwa staili ya mwendelezo kutoka Darasa la I-II na Darasa la III-VII. Aidha, unalenga kuendeleza umahiri uliojengwa na mwanafunzi kutoka darasa moja kwenda darasa lingine. Hivyo, katika kila darasa kutakuwa na kukazia ujuzi na maarifa kwa yale ambayo mwanafunzi amejifunza katika Darasa la nyuma. Muhimu ni kwamba kutakuwepo na ufuatiliaji wa karibu wa utendaji wa kila mwanafunzi katika kila darasa ili ajenge umahiri uliokusudiwa. Mtaala huu vilevile umeandaliwa kwa kuzingatia Sheria ya Elimu, matamko ya kisera, matamko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa na Kiunzi cha Mtaala wa Taifa kwa Elimu Msingi na Elimu Ualimu cha mwaka 2019.

## 2.2 Sheria ya Elimu Namba 25

Mtaala huu umezingatia maelekezo ya Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisho lake Sura ya 353 ya mwaka 2002. Sheria hii inatamka kwamba Elimu ya Msingi itatolewa kwa miaka saba na ni haki na ya lazima kwa kila mtoto. Aidha sheria hii inasisitiza kwamba kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule ataandikishwa kuanza shule na kuhudhuria kwa miaka yote saba.

## 2.3 Matamko ya Kisera

Mtaala huu umeandaliwa kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 na ya 2014. Sera ya mwaka 1995 inaelekeza kuhusu ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu pamoja na ufuatiliaji na tathimini ya Elimu ya Msingi. Maelezo yaliyomo katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 yamezingatia:

a) Matumizi zaidi ya Sayansi na Teknolojia katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote. Lengo ni kuwa na idadi ya kutosha ya wananchi walioelimika katika Sayansi na Teknolojia na kukidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa.

Hivyo, Mtaala huu unaweka umuhimu katika matumizi ya Sayansi na Teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji.

b) Mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia kwa kuhakikisha uwepo wa miundo mbinu bora na stahiki ya kutosheleza mahitaji ya elimu kwa makundi yote katika ngazi zote za elimu. Hii ni pamoja na kuwa na mazingira salama na huduma muhimu shuleni kwa lengo la kuchangia ushiriki wa waalimu na wanafunzi katika mchakato wa kupata elimu bora.

## 2.4 Matamko ya Kitaifa na Kimataifa

Haya ni matamko yenye umuhimu katika uandaaji na utoaji wa elimu nchini. Hii ni pamoja na kutekeleza mikataba mbalimbali ambayo nchi imeingia na mataifa mengine katika utoaji wa Elimu ya Msingi ambayo ni haki ya kila mtoto.

### 2.4.1 Matamko ya kitaifa

Mtaala wa Elimu ya Msingi umezingatia matamko mbalimbali ya kitaifa. Baadhi ya matamko hayo ni kama yafuatayo:

***a) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (MKUKUTA)***

Malengo yaliyomo katika MKUKUTA yamezingatiwa katika uandaaji wa mtaala huu. Malengo hayo ni yale yanayosisitiza kuwa na mtaala utakaowapa walengwa maarifa, stadi na mielekeo chanya ya kushiriki vyema katika kujiletea maendeleo yao wenyewe. Hii itasaidia katika kupunguza umaskini.

***b) Dira ya Maendeleo ya Taifa hadi mwaka 2025***

Dira hii inasisitiza utoaji wa elimu bora ili kuwajengea walengwa ubunifu, ugunduzi, maarifa na stadi mbalimbali. Pia, inalenga kutoa wataalamu wenye uwezo wa kutatua matatizo ya jamii kwa kutumia sayansi na teknolojia.

### 2.4.2 Matamko ya kimataifa

**_a) Malengo ya maendeleo ya Milenia_**

Mtaala huu, unazingatia pia malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Milenia. Kwa kuzingatia vipaumbele na hali halisi ya taifa, malengo hayo yamefupishwa katika malengo saba kama ifuatavyo:

(i) kuhakikisha elimu bora inatolewa kwa watu wote;

(ii) kuondoa umaskini na kuboresha kilimo, usalama wa chakula na lishe;

(iii) kudumisha mifumo ya maisha ili kuimarisha afya na hali bora kwa watu wa rika zote;

(iv) kudumisha haki na usawa ndani ya nchi na baina ya nchi na nchi na kuboresha makazi ya watu kuwa salama, yenye amani na yaliyo katika mifumo ya haki;

(v) kuhakikisha upatikanaji wa nishati salama, maji safi na salama na usafi wa mazingira kwa watu wote;

(vi) kuimarisha ukuzaji wa uchumi, viwanda, ugunduzi, ajira, uwiano katika uzalishaji na matumizi na ujenzi wa miundombinu; na

(vii) kuthibiti mabadiliko ya hali ya hewa, utunzaji bora wa mazingira, matumizi mazuri ya rasilimali za majini na mfumo wa ikolojia ili kuhakikisha viumbe, wanyama na mimea wanakaa pamoja kwa kutegemeana.

**_b) Sera ya Haki za Mtoto ya 1989_**

Sera za kimataifa zilizozingatiwa katika uboreshaji wa mtaala huu ni pamoja na Sera ya Haki za Mtoto ya mwaka 1989, ihusuyo mataifa kutoa elimu kwa watu wote. Mtaala umezingatia pia kuwapo kwa tamko la Maendeleo Endelevu ya Milenia la mwaka 2000, kipengele cha 2 na 3, vinavyotoa haki ya elimu kwa watoto wote na elimu ya jinsia ambayo inalenga kukuza ujifunzaji unaozingatia kuimarisha ukuaji wa uchumi na kuwa na uwiano sawa katika uzalishaji. Aidha, mtaala umezingatia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji elimu.

## 2.5 Kiunzi cha Mtaala wa Taifa kwa Elimumsingi na Elimu Ualimu

Uandaaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi umeongozwa na Kiunzi cha Mtaala wa Taifa kwa Elimu Msingi na Elimu Ualimu cha mwaka 2019. Kwanza, kiunzi hiki kinaeleza bayana dira ya elimu inayozingatia kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, ujuzi na mitazamo chanya katika kuchangia maendeleo ya taifa. Pili, kinazingatia dhima ya elimu inayosisitiza kuwa na mfumo wa utoaji wa elimu ambayo itamwezesha Mtanzania aliyeelimika kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya taifa. Tatu, kiunzi hiki vilevile kimebainisha umahiri, maeneo ya kujifunza, upimaji na usimamizi katika Elimu ya Msingi.

## 2.6 Mitazamo ya Mtaala

Uandaaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi umejikita katika mitazamo mbalimbali kama vile mtaala unaozingatia falsafa ya elimu, utamaduni, lugha, sayansi na teknolojia pamoja na elimu jumuishi.

### 2.6.1 Falsafa ya elimu

Mtaala wa Elimu ya Msingi unazingatia Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea. Falsafa hii imekuwa ndio msingi wa elimu Tanzania tangu mwaka 1967. Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea inaweka msisitizo katika mambo yafuatayo:

a) uwiano kati ya elimu na mahitaji ya jamii au walengwa;
b) kukuza fikra tunduizi na tabia za udadisi;
c) kujifunza kwa kuhusisha nadharia na vitendo;
d) kukuza kujiamini, kufanya uamuzi na kuthamini utu; na
e) kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali.

### 2.6.2 Utamaduni

Mtaala wa Elimu ya Msingi unazingatia utamaduni kama kielelezo na utambulisho wa Mtanzania. Unajumuisha ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia mila, tunu, desturi na miiko ya Mtanzania. Vilevile mtaala unalenga kumwezesha mwanafunzi kutambua na kuthamini masuala anuwai ya utamaduni wake na wa jamii nyingine.

### 2.6.3 Lugha

Lugha imepewa kipaumbele katika utoaji elimu Tanzania kwa ngazi mbalimbali za elimu. Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 inaelekeza matumizi ya Kiswahili, Kiingereza, lugha ya alama pamoja na lugha nyingine za kigeni katika elimu na mafunzo. Mtaala huu utatekelezwa kwa kutumia Kiswahili kwa masomo ya Hisabati, Uraia na Maadili, Sayansi na Teknolojia, Stadi za Kazi na Maarifa ya Jamii. Vilevile, Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu yatafundishwa kama masomo. Hivyo basi Kiswahili kitafundishwa kama somo kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia.

### 2.6.4 Sayansi, teknolojia ya habari na mawasiliano

Matumizi ya sayansi na TEHAMA yamepewa kipaumbele katika utoaji wa elimu. Mtaala huu unalenga kumpatia mwanafunzi stadi na maarifa yatakayomsaidia kujenga uwezo wa kutumia sayansi na teknolojia katika kutatua matatizo katika maisha ya kila siku. Mtaala umeweka msisitizo katika matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Wanafunzi wana fursa ya kutumia teknolojia katika kujifunza masomo yote ili kukuza stadi za kutenda na kutumia vifaa mbalimbali vya teknolojia.

### 2.6.5 Mtaala jumuishi na unaozingatia umahiri

Mtaala umejikita katika kusisitiza ujenzi wa umahiri ambao unajumuisha maarifa, stadi na mwelekeo. Umahiri katika kila darasa umeoneshwa na unalenga kukidhi mahitaji ya ukuaji wa mtoto na mahitaji ya kielimu. Mwanafunzi ni kitovu cha kujifunza na msisitizo upo katika kumwezesha jinsi ya kujifunza na kujenga tabia ya kujifunza katika maisha yake yote. Wanafunzi wenye uwezo wa juu wa kutenda na vipaji watapewa fursa ya kuviendeleza na wale wenye vikwazo katika kujifunza watapata usaidizi maalum. Mtaala huu vilevile utamwezesha mwanafunzi kujifunza kwa kushiriki shughuli mbalimbali nje ya darasa kama vile michezo, sanaa, klabu za masomo na uzalishaji mali.

# Mchakato wa Uandaaji wa Mtaala

## 3.1 Utangulizi

Kazi ya kuandaa mtaala hupitia katika hatua mbalimbali ili kupata mtaala ambao unakidhi mahitaji ya walengwa. Katika kuandaa Mtaala wa Elimu ya Msingi, hatua tatu zilizingatiwa:

## 3.2 Hatua za Kuandaa Mtaala

### 3.2.1 Tathimini ya mahitaji

Hatua hii ilihusisha kufanya utafiti wenye lengo la kukusanya maoni na mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2005 na maboresho yanayohitajika kwa mtaala mpya. Washiriki wa utafiti huu walikuwa walimu 300 kutoka mikoa 24 ya Tanzania Bara. Walishiriki pia wadau wengine wa elimu wakiwemo maafisa elimu wa wilaya na mikoa, wathibiti ubora wa shule, watunga sera na viongozi wakuu wa wizara. Aidha, walikuwemo pia maafisa kutoka asasi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali, wazazi, wanafunzi na jamii kwa ujumla. Vilevile hatua hii ilihusisha kupitia nyaraka mbalimbali. Baadhi ya nyaraka hizo ni: ripoti za mikutano ya majopo ya masomo, ripoti juu ya tahimini ya utekelezaji wa mtaala wa mwaka 2005, ripoti za tafiti mbalimbali juu ya utekelezaji wa mtaala wa mwaka 2005, mitaala ya nchi mbalimbali za ndani na nje ya Afrika na Kiunzi cha Mtaala wa Taifa kwa Elimu Msingi na Elimu Ualimu cha mwaka 2019.

### 3.2.2 Mkutano wa waratibu mitaala

Hatua hii ilihusisha mkutano wa waratibu wa mitaala wa TET ambao walipitia na kuchambua matokeo ya utafiti juu ya tahimini ya mahitaji. Matokeo ya utafiti huu yalitumika katika kuandaa Rasimu ya kwanza ya mtaala. Rasimu hiyo iliwasilishwa kwa wadau mbalimbali wa elimu na kutolewa maoni. Maoni yaliyopatikana kutoka kwa wadau yalitumika katika kuboresha rasimu ya mtaala.

### 3.2.3 Majopo ya wataalamu wa somo

Hatua hii ilihusisha majopo ya wataalamu wa masomo ambayo yalipitia rasimu ya mtaala kwa kushirikiana na waratibu wa mitaala. Mrejesho kutoka katika majopo ulitumika kufanya maboresho katika maeneo mbalimbali ya mtaala. Baada ya kuingiza mapendekezo ya majopo, utaratibu wa kuidhinisha mtaala ulifuata, ambao ulihusisha Kamati ya Taaluma ya TET, Baraza la TET na Kamishna wa Elimu.

## Ushiriki wa Wadau wa Elimu katika Uandaaji wa Mtaala

### 4.1 Utangulizi

Mafanikio ya mtaala huu yanategemea ushiriki wa wadau mbalimbali wa elimu wakiwemo wazazi, jamii, sekta ya umma na sekta binafsi. Ushiriki wa wadau hawa umefafanuliwa kama ifuatavyo.

### 4.2 Ushiriki wa Wazazi na Jamii

Malezi na maendeleo ya mtoto huanzia katika ngazi ya familia, ikisaidiana na jamii inayomzunguka. Kwa hiyo, ushiriki wa wazazi na jamii katika kuboresha elimu ni jambo muhimu kwa malezi ya mwanafunzi, hususani ushiriki wao katika kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kitaaluma, kitabia, kiustawi na kuwasaidia kujifunza. Vilevile, muhimu ni ushiriki wao katika ujenzi wa miundombinu ya shule.

### 4.3 Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi

Sekta ya Elimu ni eneo muhimu la uwekezaji kwa njia ya ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Lengo kuu la ubia huu ni kuongeza uwezo wa sekta ya Elimu katika kupanua na kuimarisha miundombinu wezeshi, taaluma, utaalamu na huduma mbalimbali katika ngazi zote za elimu na mafunzo. Serikali imeweka utaratibu wa ubia kati yake na sekta binafsi katika utekelezaji wa Elimu ya Msingi. Ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza elimu utajumuisha mambo mbalimbali yakiwemo:

a) kuwezesha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoa elimu kwa watoto wa Tanzania kwa kujenga shule zinazokidhi nia ya serikali ya kutoa elimu bora;
b) kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia;
c) kujenga miundombinu ikiwemo madarasa, maabara, maktaba na vyoo; na
d) kuchangia gharama za mafunzo kwa walimu wa shule zisizokuwa za serikali wakati wa mafunzo elekezi.

# Malengo na Umahiri katika Mtaala wa Elimu ya Msingi

## 5.1 Utangulizi

Mtaala huu umezingatia malengo yaliyoainishwa katika Kihunzi cha Mtaala wa Taifa kwa Darasa la I-II na la III-VIII. Vilevile, umahiri katika Elimu ya Msingi umezingatiwa kwa ngazi ya Darasa la I-II na la III-VII. Mazingatio hayo yamefafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

## 5.2 Malengo ya Elimu ya Msingi

Yafuatayo ndiyo malengo ya Elimu ya Msingi:

**a) Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la I-II**

Mtaala umeandaliwa ili mwanafunzi wa Darasa la I-II aweze:

(i) kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu;
(ii) kuwasiliana kwa njia sahihi;
(iii) kutunza afya na usafi;
(iv) kujenga uimara wa mwili na kushirikiana na wengine;
(v) kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza;
(vi) kuthamini mazingira;
(vii) kujitambua na kukuza vipaji;
(viii) kukua kimaadili; na
(ix) kukua kiimani kwa mujibu wa dini yake.

**b) Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VII**

Mtaala umeandaliwa ili mwanafunzi wa Darasa la III-VII aweze:

(i) kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana;
(ii) kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili;
(iii) kufahamu misingi ya utawala wa sheria;
(iv) kuthamini utamaduni wa kitanzania na wa jamii nyingine;
(v) kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kufikiri, kubuni na kutatua matatizo;
(vi) kutambua umuhimu wa maadili, uadilifu na uwajibikaji kama misingi ya raia mwema;

(vii) kushiriki katika shughuli za michezo na sanaa pamoja na kuthamini kazi za kisanii;

(viii) kubaini na kukuza vipaji na vipawa vya mwanafunzi;

(ix) kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(x) kutambua, kuthamini na kutumia sayansi na teknolojia; na

(xi) kujiandaa kwa ngazi nyingine ya elimu pamoja na kujifunza kusiko na kikomo.

## 5.3 Umahiri katika Elimu ya Msingi

Umahiri unawiana na malengo ya Elimu ya Msingi kama inavyooneshwa katika sehemu zifuatazo.

**a) Umahiri katika Darasa la I-II**

Mtaala wa Elimu ya Msingi umejikita katika umahiri ambao utamwezesha mwanafunzi wa Darasa la I-II:

(i) kusoma ;

(ii) kuandika;

(iii) kuhesabu;

(iv) kutunza afya na mazingira; na

(v) kujiendeleza katika michezo na sanaa.

**b) Umahiri katika Darasa la III-VII**

Mtaala wa Elimu ya Msingi umejikita katika umahiri ambao utamwezesha mwanafunzi wa Darasa la III-VII:

(i) kuwasiliana kwa ufasaha kwa Kiswahili na Kiingereza kwa kuzungumza na kuandika;

(ii) kusoma kwa kujiamini na kufahamu maandishi sahili;

(iii) kutumia dhana na kanuni za kihisabati katika maisha ya kila siku;

(iv) kutumia stadi za kisayansi, kiteknolojia na kiufundi katika maisha halisi ya kila siku;

(v) kutumia utamaduni wake na wa jamii nyingine kwa usahihi katika maisha ya kila siku;

(vi) kuheshimu tofauti za kiimani na kiitikadi katika jamii;

(vii) kushiriki katika michezo na shughuli za kisanii;

(viii) kujiheshimu na kuheshimu wengine;

(ix) kutumia misingi ya kizalendo katika maisha ya kila siku;

(x) kushiriki katika kazi mbalimbali zinazoendana na umri wake;

(xi) kushiriki katika shughuli zinazokuza uwezo wake wa kufikiri kimantiki na kiyakinifu; na

(xii) kushirikiana na wengine kwa kufanya matendo yanayokubalika katika jamii.

## 5.4 Walengwa wa Mtaala

Mtaala wa Elimu ya Msingi umebainisha makundi matatu ya wanafunzi wanaotakiwa kupatiwa elimu kama haki yao ya msingi. Kundi la kwanza ni wanafunzi wasio na mahitaji maalum. Kundi la pili ni la wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hawa ni wale wanaobainishwa kwa kupitia upimaji chekeche na gunduzi kuwa wanaweza kujumuishwa katika mfumo wa madarasa ya kawaida na kuwa wanaweza kufaidika kwa kujifunza pamoja na wanafunzi wasio na mahitaji maalum. Kundi la tatu ni la watoto wenye mahitaji maalum wanaobainishwa kwa upimaji chekeche na gunduzi kuwa wanahitaji mafunzo maalum ili waweze kufaidika na elimu. Hivyo, mfumo wa mafunzo kwa watoto hawa wenye mahitaji maalum utakuwa ni ule wa madarasa maalum au vitengo.

# Maeneo ya Umahiri katika Darasa la I-II

## 6.1 Utangulizi

Mtaala wa Elimu ya Msingi umezingatia maeneo matatu makuu ya umahiri ambayo ni stadi za KKK na Stadi Wezeshi kwa wanafunzi wa Darasa la I na la II. Stadi za KKK ndilo eneo la msingi na linalenga kumwezesha mwanafunzi kupata umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Eneo la Stadi Wezeshi linajikita katika stadi nyingine ambazo zikikuzwa zitamsaidia mwanafunzi kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu na kumudu maisha yake ya kila siku. Hivyo basi, maeneo haya ya kujifunza yatamjenga mwanafunzi kiafya, kimwili, kiakili na kisaikolojia kwa kushiriki katika michezo, kuchora, kuimba, kuigiza na elimu ya dini ambayo ina nafasi kubwa katika kumsaidia mwanafunzi kukua kiroho na kimaadili.

## 6.2 Umahiri katika Kusoma, Kuandika na Kuhesabu

Sehemu hii imejikita katika kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Jedwali Na. 1 na Na. 2 yanaonesha uwezo wa kutenda ambao mwanafunzi anategemewa kuujenga katika Darasa la I na la II.

**Jedwali Na. 1: Umahiri katika KKK Darasa la I**

| Kusoma | Kuandika | Kuhesabu |
|---|---|---|
| Lugha ya mazungumzo | Misingi ya kuandika | Utambuzi wa namba |
| Utambuzi wa sauti | Uumbaji wa herufi | Utambuzi wa uhusiano wa idadi ya vitu na namba |
| Utambuzi wa sauti za herufi | Matumizi ya kanuni za uandishi | Matumizi ya matendo katika namba |
| Kusoma kwa ufasaha | Ufasaha na ushikamani | Utambuzi wa vipimo |
| Ufahamu wa Kusoma na Kusikiliza | Uandishi wenye mfuatano sahihi wa matukio | Utambuzi wa maoumbo |
| Matumizi ya msamiati | Uandishi wa mwandiko wa chapa | Kukusanya na kuorodhesha vitu |

**Jedwali Na. 2: Umahiri katika KKK Darasa la II**

| Kusoma | Kuandika | Kuhesabu |
|---|---|---|
| Lugha ya mazungumzo | Uumbaji wa herufi | Kutambua namba |
| Utambuzi wa sauti | Uundaji wa maneno | Kutambua uhusiano wa idadi ya vitu na namba |
| Utambuzi wa sauti za herufi | Kuandika kwa mfuatano sahihi wa matukio | Kutumia matendo katika namba |
| Matumizi ya msamiati | Matumizi ya kanuni za uandishi | kutambua vipimo |
| Ufahamu wa kusoma na kusikiliza | Ufasaha na ushikamani | Kutambua maumbo |
| Kusoma kwa ufasaha | | Kukusanya na kuorodhesha vitu |

## 6.3 Umahiri katika Stadi Wezeshi

Eneo la stadi wezeshi limejikita katika kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri katika stadi za KKK. Jedwali Na. 3 linaonesha uwezo wa kutenda ambao mwanafunzi anategemewa kuujenga katika Darasa la I na la II.

**Jedwali Na. 3: Umahiri katika stadi wezeshi Darasa la I-II**

| Kutunza afya na mazingira | Kujiendeleza katika michezo na sanaa |
|---|---|
| Kubaini sehemu za nje za mwili wa binadamu | Kucheza michezo sahili |
| Kubaini njia za kujikinga na magonjwa | Kuonesha mwenendo sahihi katika michezo |
| Kusafisha na kutunza mazingira | Kufuata kanuni katika michezo na sanaa |
| Kutoa huduma ya kwanza | Kuwasiliana kupitia sanaa |
| Kutambua viumbe hai | Kubuni na kuimarisha stadi za michezo na sanaa |

## 6.4 Muda wa Kufundisha na Idadi ya Vipindi Darasa la I-II

Mwaka wa shule utakuwa na siku 194 ambazo ni sawa na wiki 39. Mwaka umegawanywa katika mihula miwili; hivyo kutakuwa na mihula miwili (2) ya masomo. Katika kila muhula wiki mbili (2) zitatumika kwa upimaji. Ili kufikia malengo ya mtaala huu na kupata matokeo yanayotarajiwa, mwanafunzi wa Darasa la I na la II atasoma stadi sita (6). Stadi hizo ni Kusoma, Kuandika, Kuhesabu, Kutunza Afya na Mazingira, Kujiendeleza katika Michezo na Sanaa pamoja na Elimu ya Dini. Muda wa kufundisha kwa wiki ni saa 15 na kutakuwa na vipindi sita (6) kwa siku. Muda wa kila kipindi utakuwa wa dakika 30 tu. Hivyo katika siku moja ya mafunzo itampasa mwanafunzi kujifunza kwa muda wa saa 3 tu. Mgawanyo huu wa muda unaonesha kwamba eneo la Kusoma, Kuandika na Kuhesabu linachukua 80%, eneo la Stadi Wezeshi linachukua 13% na Elimu ya dini itachukuwa 7% ya muda wote wa kujifunza. Jedwali Na. 4 linaonesha muda wa kufundisha na kujifunza kwa kila somo.

**Jedwali Na. 4: Mgawanyo wa muda na vipindi kwa Darasa la I-II**

| Somo | Idadi ya saa kwa wiki | Idadi ya vipindi kwa wiki |
|---|---|---|
| Kusoma | 5 | 10 |
| Kuandika | 3 | 6 |
| Kuhesabu | 4 | 8 |
| Kutunza Afya na Mazingira | 1 | 2 |
| Kuendeleza Michezo na Sanaa | 1 | 2 |
| Elimu ya Dini | 1 | 2 |
| **Jumla** | **15** | **30** |

# Maeneo ya Kujifunza Darasa la III - VII

## 7.1 Utangulizi

Sehemu hii inaonesha maeneo makuu sita ya kujifunza na manufaa yake katika kujifunza kwa wanafunzi wa Darasa la III-VII. Maeneo hayo ni: lugha, sayansi ya jamii, sayansi na teknolojia, hisabati, michezo na sanaa na masuala ya kiroho.

## 7.2 Maeneo Makuu ya Kujifunza

### 7.2.1 Lugha

Lugha ni msingi muhimu wa maendeleo ya mwanadamu na utambulisho wa utamaduni wake. Lugha humwezesha mwanafunzi kuwasiliana katika shughuli za kila siku katika miktadha na mazingira mbalimbali. Umahiri wa lugha humwezesha pia mwanafunzi kujifunza kwa ufanisi. Msisitizo katika lugha ni kumwandaa mwanafunzi mwenye umahiri wa kusikiliza, kusoma, kuzungumza na kuandika kwa ufasaha Kiswahili na Kiingereza. Hivyo, mwanafunzi atajifunza na kuwa na uelewa wa jumla wa kujieleza kwa kutumia lugha inayojumuisha alama. Mwanafunzi, vilevile, anayo fursa ya kuchagua kujifunza Kifaransa au Kiarabu kwani lugha hizi zinaonekana kuwa muhimu katika biashara, uhusiano na utalii.

### 7.2.2 Sayansi ya jamii

Eneo hili la masomo ya sayansi ya jamii linahusisha Somo la Maarifa ya Jamii na la Uraia na Maadili. Kujifunza sayansi ya jamii kunalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa na maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kutekeleza wajibu wake katika jamii na kuchangia katika maendeleo. Eneo hili linamjengea mwanafunzi uwezo wa kuelewa na kuthamini haki za binadamu na umuhimu wake, kuelewa historia ya jamii na kutekeleza wajibu wake katika jamii. Sayansi ya jamii humwezesha mwanafunzi kuelewa, kuthamini na kuendeleza utamaduni unaofaa katika jamii pamoja na kutambua tamaduni za jamii nyingine zinazofaa.

Vilevile, eneo hili la masomo humwezesha mwanafunzi kuyaelewa mazingira anamoishi, kuyatunza, kuyahifadhi na kuyatumia katika njia endelevu. Aidha, humwezesha mwanafunzi kutambua na kushiriki katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

### 7.2.3 Sayansi na teknolojia

Eneo hili linahusisha maarifa na stadi za kisayansi zitakazomwezesha mwanafunzi kupenda na kutumia misingi ya sayansi na teknolojia katika maisha ya kila siku. Sayansi na teknolojia inamjengea mwanafunzi uwezo wa kufikiri kiyakinifu kutakakomwezesha kumudu maisha ya kila siku. Kupitia sayansi mwanafunzi atajenga umahiri wa kutafuta suluhisho linaloweza kutatua matatizo katika mazingira tofauti.

### 7.2.4 Hisabati

Hisabati ni nyenzo muhimu katika kukuza na kuimarisha kufikiri kiyakinifu, kimantiki, kinadharia na kidhahania. Mwanafunzi atajenga uwezo wa kutumia mbinu mbalimbali katika kutatua baadhi ya changamoto anazokutana nazo katika maisha. Hii yote hufanyika katika nyanja zote za maisha na maendeleo ya binadamu. Aidha, katika Somo la Hisabati mwanafunzi atakuza stadi zinazotumika kujifunzia masomo mengine.

### 7.2.5 Michezo na sanaa

Eneo hili linagusa umahiri muhimu katika maisha ya kila siku. Masomo ya eneo hili yanalenga kumwezesha mwanafunzi kupenda na kujihusisha katika kazi za mikono. Masomo haya yatajenga stadi za awali za kufanya kazi. Kushiriki katika michezo na sanaa kunawafanya wanafunzi kujenga miili yenye afya na hasa ukizingatia mabadiliko ya mfumo wa maisha ambapo watu wengi wanazidi kutumia muda mdogo katika mazoezi ya mwili. Aidha, masomo haya yanakuza stadi za ubunifu, ushirikiano, utatuzi wa matatizo na ukuzaji wa vipaji. Eneo hili la masomo ya vitendo linahusisha Somo la Stadi za Kazi na la Michezo na Sanaa.

### 7.2.6 Masuala ya dini

Hili ni eneo linalohusika na kumwezesha mwanafunzi kujenga tabia za uadilifu, uvumilivu na kuheshimu tofauti za kiimani na za kiitikadi wakati wote na mahali popote. Kupitia somo la Elimu ya Dini mwanafunzi atajenga mwenendo unaokubalika katika jamii kwa kuimarisha uwezo wa kufikiri kiyakinifu na kutatua matatizo kwa kuzingatia misingi ya dini.

## 7.3 Mgawanyo wa Masomo

Wanafunzi wa Darasa la III na IV watajifunza masomo saba na wanafunzi wa Darasa la V hadi VII watajifunza masomo nane kama yanavyooneshwa katika Jedwali Na. 5.

**Jedwali Na. 5: Mgawanyo wa masomo kwa Darasa la III - VII**

| Na | Masomo ya Darasa la III– IV | Na | Masomo ya Darasa la V-VII |
|---|---|---|---|
| 1 | Kiswahili | 1 | Kiswahili |
| 2 | Kiingereza | 2 | Kiingereza |
| 3 | Hisabati | 3 | Hisabati |
| 4 | Sayansi na Teknolojia | 4 | Sayansi na Teknolojia |
| 5 | Maarifa ya Jamii | 5 | Maarifa ya Jamii |
| 6 | Uraia na Maadili | 6 | Uraia na Maadili |
| 7 | Elimu ya Dini | 7 | Stadi za Kazi |
| | | 8 | Elimu ya Dini |

Kutakuwa na masomo chaguzi na shughuli za nje ya darasa. Masomo chaguzi ya Kiarabu na Kifaransa yatafundishwa kwenye shule zenye uwezo na vifaa vya kufundishia masomo hayo. Shughuli za nje ya darasa au mtaala wa ziada zitahusisha klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza. Maeneo hayo ni sanaa, michezo, kazi za uzalishaji mali, kujisomea na burudani kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Masomo ya kuchagua katika Mtaala wa Ziada**

| Na. | Masomo chaguzi | Shughuli za mtaala wa ziada |
|---|---|---|
| 1 | Kiarabu | Klabu za Masomo |
| 2 | Kifaransa | Michezo na Sanaa |
| 3 | | Uzalishaji Mali |
| 4 | | Kujisomea na Burudani |

## 7.4 Umahiri katika Masomo

Mtaala wa Elimu ya Msingi umezingatia umahiri mkuu na umahiri mahususi katika kila somo. Kila Umahiri Mkuu katika somo umegawanywa katika Umahiri Mahususi kwa Darasa la III-IV na Darasa la V-VII.

### 7.4.1 Kiswahili

Umahiri katika Somo la Kiswahili umegawanywa kimadarasa. Ugawaji wa umahiri mkuu na umahiri mahususi katika Darasa la III-IV ni mwendelezo wa umahiri mkuu na umahiri mahususi uliojengwa kutoka Darasa la I-II katika stadi za Kusoma na Kuandika. Jedwali Na. 7 limebainisha umahiri mkuu na umahiri mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika Somo la Kiswahili kuanzia Darasa la III - VII.

**Jedwali Na. 7: Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Kiswahili**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III-IV | Umahiri mahususi Darasa la V-VII |
|---|---|---|
| 1.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kutambua sauti mbalimbali katika matamshi ya silabi, maneno, sentensi na habari<br>1.2 Kutumia matamshi sahihi katika kutamka maneno mbalimbali | 1.1 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali<br>1.2 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III-IV | Umahiri mahususi Darasa la V-VII |
|---|---|---|
| | 1.3 Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali<br>1.4 kutumia msamiati katika kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali<br>1.5 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali<br>1.6 Kutumia msamiati katika uandishi wa matini mbalimbali | 1.3 Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali<br>1.4 Kutumia msamiati katika uandaaji na uandishi wa matini mbalimbali |
| 2.0 Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma. | 2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza<br>2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyosoma<br>2.3 Kutumia msamiati aliousoma ili kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika miktadha mbalimbali | 2.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza<br>2.2 Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma<br>2.3 Kutumia msamiati aliousoma katika kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III-IV | Umahiri mahususi Darasa la V-VII |
|---|---|---|
| 3.0 Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali. | 3.1 Kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali<br>3.2 Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali<br>3.3 Kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali | 3.1 Kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali<br>3.2 Kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali<br>3.3 Kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali |

### 7.4.2 Kiingereza

Umahiri katika Somo la Kiingereza umegawanyika katika madarasa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Kiingereza**

| Main competences | Specific competences Standard III | Specific competences Standard IV-VII |
|---|---|---|
| 1.0 Comprehend oral and written information | 1.1 Listen and comprehend information presented orally<br>1.2 Listen and comprehend phonemic symbols<br>1.3 Listen, pronounce and read phonemic symbols | 1.1 Listen and comprehend information presented orally<br>1.2 Read and comprehend written information |

| Main competences | Specific competences Standard III | Specific competences Standard IV-VII |
|---|---|---|
| 2.0 Communicate orally and through writing | 2.1 Communicate simple ideas through speaking<br>2.2 Communicate simple ideas through writing | 2.1 Communicate simple ideas through speaking<br>2.2 Communicate simple ideas through writing |
| 3.0 Use appropriate vocabulary through the four language skills (Listening, speaking, reading and writing) | 3.1 Develop and use appropriate vocabulary through listening and speaking.<br>3.2 Develop and use vocabulary through reading<br>3.3 Use appropriate vocabulary when writing | 3.1 Develop and use appropriate vocabulary through listening and speaking<br>3.2 Develop vocabulary through reading<br>3.3 Use appropriate vocabulary when writing |

### 7.4.3 Hisabati

Umahiri katika Somo la Hisabati umegawanywa kimadarasa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9: Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Hisabati**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III-IV | Umahiri mahususi Darasa la V-VII |
|---|---|---|
| 1.0 Kutumia lugha ya kihisabati kuwasilisha wazo au hoja katika maisha ya kila siku | 1.1 Kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti<br>1.2 Kutumia stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali | 1.1 Kutumia dhana ya namba kuwasiliana katika mazingira tofauti<br>1.2 Kutumia stadi za aljebra kutatua matatizo katika maisha ya kila siku |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi<br>Darasa la III-IV | Umahiri mahususi<br>Darasa la V-VII |
|---|---|---|
| | | 1.3 Kutumia stadi za takwimu kuwasilisha taarifa mbalimbali |
| 2.0 Kufikiri na kuhakiki kihisabati vitu mbalimbali katika maisha ya kila siku | 2.1 Kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali<br>2.2 Kutumia stadi za maumbo katika maisha ya kila siku<br>2.3 Kutumia stadi za mpangilio kufumbua mafumbo katika maisha ya kila siku | 2.1 Kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali<br>2.2 Kutumia stadi za maumbo kufumbua mafumbo katika miktadha ya kihisabati<br>2.3 Kutumia stadi za mpangilio kufumbua mafumbo katika maisha ya kila siku |
| 3.0 Kutumia hisabati kutatua matatizo katika mazingira tofauti | 3.1 Kutumia matendo ya namba ya kihisabati katika kutatua matatizo<br>3.2 Kutumia stadi za uhusiano wa namba na vitu katika kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali | 3.1 Kutumia matendo ya namba ya kihisabati katika kutatua matatizo<br>3.2 Kutumia stadi za uhusiano wa namba na vitu katika kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali |

### 7.4.4 Sayansi na Teknolojia

Umahiri katika Somo la Sayansi na Teknolojia umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na.10.

**Jedwali Na.10: Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Sayansi na Teknolojia**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III-IV | Umahiri mahususi Darasa la V-VII |
|---|---|---|
| 1.0 Kufanya uchunguzi na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia | 1.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira<br>1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake<br>1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia | 1.1 Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira<br>1.2 Kutambua aina anuai za nishati na matumizi yake<br>1.3 Kutambua nadharia za kisayansi na kiteknolojia |
| 2.0 Kufahamu misingi ya Sayansi na Teknolojia | 2.1 Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)<br>2.2 Kumudu stadi za kisayansi<br>2.3 Kufanya majaribio ya kisayansi kwa usahihi | 2.1 Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)<br>2.2 Kumudu stadi za kisayansi<br>2.3 Kufanya majaribio ya kisayansi kwa usahihi |
| 3.0 Kutunza afya na mazingira | 3.1 Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora<br>3.2 Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora<br>3.3 Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu | 3.1 Kufuata kanuni za usafi ili kuwa na afya na mazingira bora<br>3.2 Kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora<br>3.3 Kutambua mifumo mbalimbali ya mwili wa binadamu |

### 7.4.5 Maarifa ya Jamii

Umahiri katika Somo la Maarifa ya Jamii umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye jedwali Na 11.

**Jedwali Na.11: Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Maarifa ya Jamii**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III – IV | Umahiri mahususi Darasa la V – VII |
|---|---|---|
| 1.0 Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka | 1.1 Kutunza mazingira ya jamii inayomzunguka<br>1.2 Kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria | 1.1 Kutunza mazingira ya jamii inayomzunguka<br>1.2 Kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria<br>1.3 Kutumia elimu ya hali ya hewa katika kutekeleza shughuli za kila siku |
| 2.0 Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii | 2.1 Kudumisha utamaduni wa Mtanzania<br>2.2 Kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka<br>2.3 Kuthamini mashujaa wetu | 2.1 Kufuata misingi ya utamaduni wa Mtanzania<br>2.2 Kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka<br>2.3 Kuthamini mashujaa wetu |
| 3.0 Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku | 3.1 Kutumia ramani katika mazingira.<br>3.2 Kuelezea mfumo wa jua | 3.1 Kutumia ramani katika mazingira<br>3.2 Kuelezea mfumo wa jua |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III – IV | Umahiri mahususi Darasa la V – VII |
|---|---|---|
| 4.0 Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali | 4.1 Kutumia kanuni za kiuchumi kulinda rasilimali za nchi<br>4.2 Kubaini shughuli za uzalishaji mali katika jamii<br>4.3 Kutumia stadi za ujasiriamali katika shughuli za kila siku | 4.1 Kutumia kanuni za kiuchumi kulinda rasilimali za nchi<br>4.2 Kubaini shughuli za uzalishaji mali katika maendeleo ya jamii<br>4.3 Kutumia stadi za ujasiriamali katika shughuli za kila siku |

### 7.4.6 Stadi za Kazi

Umahiri katika Somo la Stadi za Kazi umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 12.

**Jedwali Na. 12: Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Stadi za Kazi**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuwa nadhifu | 1.1 Kujenga tabia ya usafi wa mwili<br>1.2 Kutunza mavazi katika kudumisha usafi<br>1.3 Kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi |
| 2.0 Kumudu mapishi mbalimbali | 2.1 Kutambua kanuni zinazohitajika katika mapishi mbalimbali<br>2.2 Kutayarisha vyakula vya aina mbalimbali<br>2.3 Kutengeneza vinywaji mbalimbali |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 3.0 Kusanifu kazi za sanaa | 3.1 Kumudu misingi ya uimbaji na uigizaji<br>3.2 Kutengeneza picha zenye ujumbe mbalimbali kwa jamii<br>3.3 Kubuni chapa mbalimbali za sanaa za ufundi<br>3.4 Kufinyanga maumbo mbalimbali<br>3.5 Kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi mbalimbali yanayopatikana katika mazingira |
| 4.0 Kutumia stadi za ujasiriamali | 4.1 Kujenga utayari wa kujifunza<br>4.2 Kutafuta masoko ya bidhaa ndogondogo<br>4.3 Kutumia kanuni za usimamizi wa fedha |

### 7.4.7 Uraia na Maadili

Umahiri katika Somo la Uraia na Maadili umegawanywa kimadarasa. Jedwali Na. 13 limebainisha umahiri mkuu na mahususi utakaojengwa na mwanafunzi katika Somo la Uraia na Maadili kuanzia Darasa la III-VII.

**Jedwali Na. 13: Mgawanyo wa umahiri katika Somo la Uraia na Maadili**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III – IV | Umahiri mahususi Darasa la V – VII |
|---|---|---|
| 1.0 Kuheshimu jamii | 1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine<br>1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake<br>1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake | 1.1 Kujipenda na kuwapenda watu wengine<br>1.2 Kuipenda na kujivunia shule yake |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III – IV | Umahiri mahususi Darasa la V – VII |
|---|---|---|
| | | 1.3 Kuipenda Tanzania kwa kuenzi tunu za nchi na asili yake |
| 2.0 Kuithamini jamii | 2.1 Kujijali na kuwajali wengine<br>2.2 Kutunza mazingira na vilivyomo<br>2.3 Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii | 2.1 Kujijali na kuwajali wengine<br>2.2 Kutunza mazingira na vilivyomo<br>2.3 Kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii |
| 3.0 Kuwa mwajibikaji | 3.1 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi<br>3.2 Kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni<br>3.3 Kutii sheria na kanuni mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku<br>3.4 Kuwa na nidhamu binafsi<br>3.5 Kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni | 3.1 Kulinda rasilimali na maslahi ya nchi<br>3.2 Kusimamia majukumu yanayomhusu nyumbani na shuleni<br>3.3 Kutii sheria na kanuni mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku<br>3.4 Kuwa na nidhamu binafsi<br>3.5 Kushirikiana katika kutekeleza majukumu ya nyumbani na shuleni |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III – IV | Umahiri mahususi Darasa la V – VII |
|---|---|---|
| 4.0 Kuwa mstahimilivu | 4.1 Kuvumilia katika maisha ya kila siku<br>4.2 Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya<br>4.3 Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu | 4.1 Kuvumilia katika maisha ya kila siku<br>4.2 Kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya<br>4.3 Kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu |
| 5.0 Kuwa mwadilifu | 5.1 Kuaminika katika jamii<br>5.2 Kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli<br>5.3 Kusimamia haki | 5.1 Kuaminika katika jamii<br>5.2 Kutimiza majukumu yake kwa uwazi na ukweli<br>5.3 Kusimamia haki |
| 6.0 Kudumisha amani | 6.1 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti<br>6.2 Kubaini tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti<br>6.3 Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine | 6.1 Kuchangamana na watu wenye asili tofauti<br>6.2 Kubaini tofauti za kiutamaduni na mitazamo miongoni mwa watu wa jamii tofauti<br>6.3 Kujenga urafiki mwema na mataifa mengine |

### 7.4.8 Elimu ya Dini

Umahiri katika Somo la Elimu ya Dini utabainishwa na dini/dhehebu husika na utazingatia mahitaji ya mwanafunzi wa darasa husika. Umahiri huu utatumika katika kuandaa muhtasari wa Elimu ya Dini husika kwa kushirikiana TET.

### 7.4.9 Kifaransa

Umahiri katika somo la Kifaransa umegawanyika katika madarasa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 14.

**Jedwali Na. 14: Mgawanyiko wa umahiri katika somo la Kifaransa**

| Compétences principales | Compétences spécifiques III – IV | Compétences spécifiques V – VII |
|---|---|---|
| 1.0 Comprendre à l'oral et à l'écrit des informations dans des situations diverses | 1.1 Ecouter et comprendre des documents sonores dans des situations diverses de communication<br>1.2 Lire et comprendre des informations écrites (textes, annonces, sms, etc.) dans des occasions diverses | 1.1 Ecouter et comprendre des documents sonores dans des situations de communication diverses<br>1.2 Lire et comprendre des informations écrites (textes, annonces, sms, etc.) dans des occasions diverses |
| 2.0 S'exprimer à l'oral et à l'écrit dans des situations diverses | 2.1 S'exprimer à l'oral dans des situations diverses de communications.<br>2.2 Ecrire des textes courts, des messages, de petites annonces, etc | 2.1 S'exprimer à l'oral dans des situations diverses de communications<br>2.2 Ecrire des textes courts, des messages, de petites annonces, etc |

| Compétences principales | Compétences spécifiques III – IV | Compétences spécifiques V – VII |
|---|---|---|
| 3.0 Produire des textes à l'oral et à l'écrit en utilisant le vocabulaire acquis dans de différentes situations | 3.1 Produire des textes à l'oral en réutilisant le vocabulaire acquis dans des situations diverses<br>3.2 Produire des textes à l'écrit des textes et des messages en réutilisant le vocabulaire acquis dans des situations diverses<br>3.3 Réutiliser le vocabulaire acquis pour lire et comprendre des textes simples, de petites annonces, des messages, etc. avec des mots connus | 3.1 Produire des textes à l'oral en réutilisant le vocabulaire acquis dans des situations diverses<br>3.2 Produire des textes à l'écrit des textes et des messages en réutilisant le vocabulaire acquis dans des situations diverses<br>3.3 Réutiliser le vocabulaire acquis pour lire et comprendre des textes simples, de petites annonces, des messages, etc. avec des mots connus |

### 7.4.10 Kiarabu

Umahiri katika somo la Kiarabu umegawanyika katika madarasa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 15a na tafsiri yake katika Jedwali Na.15b

اللغة العربية: 15 a

المهارات في اللغة العربية موزعة على حسب الفصول كما هو موضح في الجدول 15.

الجدول رقم 15: توزيع المهارات في اللغة العربية للصف الثالث إلى السابع الإبتدائي.

| | المهارات الرئيسية | المهارات الخاصة للصف الثالث إلى الرابعة | المهارات الخاصة للصف الخامس إلى السابع |
|---|---|---|---|
| 1.0 | معرفة وفهم الحروف نطقا وكتابة | 1 استماع ونطق الحروف الهجائية عن طريق المشافهة.<br>2 فهم الحروف الهجائية وتعلقها بأصوات مختلفة.<br>3 استماع ونطق وقراءة الحروف الهجائية مع تمييز الأصوات المختلفة. | 1 استماع وفهم التعبيرات عن طريق المشافهة.<br>2 القراءة وفهم المحتوى من النصوص. |
| 2.0 | التواصل مشافهة ومن خلال الكتابة | 1 التواصل بعبارات بسيطة من خلال الكلام.<br>2 التواصل بعبارات بسيطة من خلال الكتابة. | 1 التواصل بعبارات بسيطة من خلال الكلام.<br>2 التواصل بعبارات بسيطة من خلال الكتابة. |
| 3.0 | اكتساب واستخدام المصطلحات اللغوية من خلال المهارات اللغوية الأربعة | 1 تنمية المفردات اللغوية واستخدامها من خلال الإستماع والكلام في المقتضيات المختلفة.<br>2 تنمية المفردات اللغوية واستخدامها من خلال القراءة.<br>3 استخدام المفردات المناسبة عند الكتابة. | 1 تنمية المفردات اللغوية واستخدامها من خلال الإستماع والكلام.<br>2 تنمية المفردات اللغوية واستخدامها من خلال القراءة.<br>3 استخدام المفردات المناسبة عند الكتابة |

**Jedwali Na. 15b: Tafsiri ya Jedwali Na.15a: Kiarabu kwenda Kiswahili**

| Na | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III-IV | Uhahiri mahususi Darasa la V-VII |
|---|---|---|---|
| 01 | Kuonesha uelewa wa herufi kwa kutamka na kuandika | 1.1 Kusikiliza na kutamka herufi za Kiarabu kwa njia ya mazungumzo<br>1.2 Kuonesha uelewa wa herufi kwa kuhusianisha na sauti mbalimbali<br>1.3 Kusikiliza, kutamka, kusoma herufi na kubaini sauti mbalimbali | 1.1 Kusikiliza na kuonesha uelewa wa sentensi mbalimbali kwa njia ya mazungumzo<br>1.2 Kusoma na kuonesha uelewa wa matini aliyosoma |

| Na | Umahiri mkuu | Umahiri mahususi Darasa la III-IV | Uhahiri mahususi Darasa la V-VII |
|---|---|---|---|
| 02 | Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandishi | 2.1 Kuwasiliana kwa kutumia sentensi mbalimbali kwa njia ya mazungumzo<br>2.2 Kuwasiliana kwa kutumia sentensi mbalimbali kwa njia ya maandishi | 2.1 Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo kwa kutumia sentensi mbalimbali<br>2.2 Kuwasiliana kwa njia ya maandishi kwa kutumia sentensi mbalimbali |
| 03 | Kutumia misamiati ya lugha kwa kupitia umahiri wa stadi nne za lugha | 3.1 Kukuza na kutumia misamiati ya lugha kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza katika miktadha mbalimbali<br>3.2 Kukuza misamiati ya lugha kwa njia ya kusoma na kuitumia katika miktadha mbalimbali<br>3.3 Kutumia misamiati stahili katika uandishi | 3.1 Kukuza misamiati ya lugha kwa njia ya kusikiliza na kuzungumza na kuitumia katika miktadha mbalimbali.<br>3.2 Kukuza misamiati ya lugha kwa njia ya kuisoma na kuitumia katika miktadha mbalimbali<br>3.3 Kutumia misamiati stahili katika uandishi |

# Masuala Mtambuka

## 8.1 Utangulizi

Masuala mtambuka ni miongoni mwa mambo muhimu yanayozingatiwa katika Mtaala wa Elimu ya Msingi. Masuala haya yamechopekwa katika masomo mbalimbali kama masomo bebezi kulingana na ngazi ya elimu inayohusika na uelewa wa mwanafunzi. Vilevile, yapo masomo ambamo masuala mtambuka yanachopekwa wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji. Masomo hayo ni pamoja na Hisabati, Kiswahili na Kiingereza. Mgawanyo wake kidarasa umefafanuliwa katika Jedwali Na.16.

**Jedwali Na. 16: Mgawanyo wa masuala mtambuka kulingana na somo bebezi na darasa linalohusika.**

| Na. | Suala mtambuka | Masomo bebezi | Darasa linalohusika | |
|---|---|---|---|---|
| | | | III – IV | V – VII |
| 1 | Virusi vya Upungufu wa Kinga Mwilini (VVU) na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) | Sayansi na Teknolojia<br>Uraia na Maadili | √<br>√ | √<br>√ |
| 2 | Elimu ya usalama barabarani | Uraia na Maadili | √ | √ |
| 3 | Haki na wajibu wa mtoto | Uraia na Maadili | √ | √ |
| 4 | Elimu ya jinsia | Uraia na Maadili | √ | √ |
| 5 | Stadi za maisha | Uraia na Maadili<br>Stadi za Kazi<br>Maarifa ya Jamii | √<br>–<br>√ | √<br>√ |
| 6 | Elimu ya afya ya uzazi | Sayansi na Teknolojia | √ | √ |
| 7 | Elimu kuhusu rushwa | Uraia na Maadili | √ | √ |
| 8 | Elimu ya stadi za ujasiriamali | Stadi za Kazi<br>Maarifa ya Jamii | –<br>√ | √<br>√ |
| 9 | Elimu ya fedha | Stadi za Kazi<br>Hisabati | –<br>√ | √<br>√ |

| Na. | Suala mtambuka | Masomo bebezi | Darasa linalohusika | |
|---|---|---|---|---|
| | | | III – IV | V – VII |
| 10 | Elimu kuhusu dawa za kulevya | Uraia na Maadili<br>Sayansi na Teknolojia | √<br>√ | √<br>√ |
| 11 | Elimu ya mazingira | Maarifa ya Jamii<br>Sayansi na Teknolojia<br>Elimu ya Dini | √<br>√<br>√ | √<br>√<br>√ |
| 12 | Elimu ya amani | Uraia na Maadili<br>Elimu ya Dini | √<br>√ | √<br>√ |
| 13 | Elimu ya usalama wa mitandao | Sayansi na Teknolojia<br>Uraia na Maadili | √<br>√ | √<br>√ |
| 14 | Elimu ya utandawazi | Sayansi na Teknolojia<br>Uraia na Maadili | √<br>√ | √<br>√ |
| 15 | Elimu ya kodi | Uraia na Maadili<br>Maarifa ya Jamii | √<br>√ | √<br>√ |

## 8.2 Uchopekaji wa Masuala Mtambuka katika Mtaala

Masuala mtambuka mbalimbali yamechopekwa katika masomo bebezi. Jedwali Na.17 linaonesha suala mtambuka na umahiri ambao unapaswa kujengwa katika suala hilo.

**Jedwali Na. 17: Umahiri katika masuala mtambuka kimadarasa**

| Suala mtambuka | Umahiri kimadarasa | |
|---|---|---|
| | III - IV | V- VII |
| Elimu ya mazingira | a) Kusaidia kusafisha mazingira<br>b) Kushiriki kutunza mazingira yanayomzunguka | a) Kusaidia kufanya mazingira kuwa ya kijani<br>b) Kushiriki katika shughuli za kuzuia uharibifu wa mazingira<br>c) Kusaidia kutunza viumbe hai waliomo katika mazingira yake |

| Suala mtambuka | Umahiri kimadarasa | |
|---|---|---|
| | III - IV | V- VII |
| Elimu ya VVU na UKIMWI | a) Kubainisha VVU na UKIMWI.<br>b) Kuonesha upendo kwa watu wanaoishi na VVU. | a) Kuchukua tahadhari, kujikinga na kuwakinga wengine na maambukizi ya VVU.<br>b) Kuwajali watu wanaoishi na VVU. |
| Elimu ya usalama wa mtandao | Kutumia simu, luninga, redio na magazeti kwa umakini | Kutumia kompyuta, baruapepe na mitandao ya kijamii kwa umakini |
| Elimu ya Utandawazi | Kutumia utandawazi kwa faida | Kutumia utandawazi kwa faida |
| Madawa ya kulevya. | Kuchambua athari za matumizi ya madawa ya kulevya | Kuchambua njia mbalimbali za kujiepusha na matumizi ya madawa ya kulevya kwa kushirikiana na jamii |
| Elimu ya afya ya uzazi | Kutunza mwili na via vya uzazi | a) Kubainisha madhara ya ngono<br>b) Kufuata kanuni za kuepuka vitendo vya ngono ili kuepuka magonjwa na mimba za utotoni |
| Stadi za maisha | a) Kufuata kanuni za kujitambua<br>b) Kutumia kanuni na taratibu za kujiheshimu na kuheshimu wengine | a) Kufuata kanuni katika kufanya maamuzi sahihi mara kwa mara<br>b) Kushirikiana na wengine katika mambo mbalimbali<br>c) Kutumia kanuni au misingi ya kukabiliana na msongo wa mawazo |

| Suala mtambuka | Umahiri kimadarasa | |
|---|---|---|
| | III - IV | V- VII |
| Elimu ya stadi za ujasiriamali | a) Kutumia rasilimali za nyumbani kwa njia endelevu.<br>b) Kushiriki katika kutambua fursa za kiuchumi zinazopatikana katika mazingira yake | a) Kubaini fursa za kiuchumi zinazomzunguka.<br>b) Kutumia fursa za kiuchumi kujikimu |
| Elimu ya fedha | a) Kubaini muundo wa fedha ya Tanzania<br>b) Kujenga tabia ya kutunza fedha | a) Kutumia fedha kwa welevu.<br>b) Kuhifadhi fedha kwa njia rasmi, mfano katika benki au simu |
| Elimu ya amani | a) Kufasili dhana ya amani.<br>b) Kufuata taratibu za kuepuka ugomvi | a) Kutunza amani.<br>b) Kubaini athari za kukosekana amani |
| Elimu ya usalama barabarani | a) Kutumia barabara kwa usahihi.<br>b) Kubaini alama zinazomsaidia mtumiaji kutumia barabara kwa usalama | a) Kubaini alama na ishara za usalama barabarani.<br>b) Kutumia barabara, vyombo, alama, pamoja na ishara zake |
| Haki na wajibu wa mtoto | a) Kuchambua haki za msingi za mtoto.<br>b) Kubaini wajibu wa mtoto | a) Kubaini madhara ya kutowajibika kama mtoto.<br>b) Kufuata kanuni za namna ya kudai haki za mtoto |
| Elimu ya jinsia | a) Kubaini jinsi yake.<br>b) Kubainisha tofauti za kijinsia | a) Kuchambua uhusiano wa kijinsia.<br>b) Kubaini dhima ya jinsia |

| Suala mtambuka | Umahiri kimadarasa | |
|---|---|---|
| | **III - IV** | **V- VII** |
| Elimu kuhusu rushwa | Kufasili dhana ya rushwa | a) Kubaini vitendo vya rushwa na madhara yake.<br>b) Kuonesha vitendo vya kukabiliana na rushwa |
| Elimu ya kodi | Kufasili dhana ya kodi | a) Kubaini aina za kodi.<br>b) Kubaini faida za kulipa kodi<br>c) Kuonesha mwelekeo wa kupenda kulipa kodi |

# Mgawanyo wa Muda wa Kufundisha Masomo kwa Darasa la III-VII

## 9.1 Utangulizi

Muda wa wanafunzi kufundishwa/kujifunza katika mwaka wa shule umegawanyika katika idadi ya mihula, wiki, siku na vipindi. Hatimae muda huu umegawanywa baina ya kila somo na shughuli zilizo katika Mtaala wa Ziada.

## 9.2 Mgawanyo wa Muda

Mwaka wa shule utakuwa na siku 194 ambazo ni sawa na wiki 39 kwa Darasa la III-VI. Darasa la VII watakuwa na wiki 34 kutokana na darasa hilo kuwa na mtihani wa mwisho mwezi Septemba kila mwaka. Mwaka umegawanywa katika mihula miwili ya masomo. Kila muhula utakuwa na wiki mbili zitakazotumika kwa mitihani. Muda wa kusoma utakuwa ni saa 6 kwa siku kwa Darasa la III-VII. Muda wa kipindi ni dakika 40. Kutakuwa na vipindi 8 kwa siku kwa wanafunzi wote isipokuwa siku ya Ijumaa ambayo itakuwa na vipindi 6. Kwa hiyo wanafunzi watasoma vipindi 38 kwa wiki. Katika shule zinazofundisha masomo ya kuchagua, mwanafunzi atajifunza somo moja chaguzi. Somo hilo litakuwa na vipindi 2 kwa wiki. Hivyo wanafunzi hawa watasoma vipindi 40 kwa wiki. Jedwali Na. 18 linafafanua muda wa kufundisha mwanafunzi na idadi ya vipindi kwa wiki katika masomo yote yatakayofundishwa darasani na nje ya darasa.

**Jedwali Na. 18 : Muda na idadi ya vipindi kwa kila somo katika wiki**

| Na | Somo | Muda na idadi ya vipindi katika wiki | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Darasa la III-IV | | Darasa la V-VII | |
| | | Muda | Idadi ya vipindi | Muda | Idadi ya vipindi |
| 1 | Kiswahili | Saa 3 dakika 20 | 5 | Saa 3 dakika 20 | 5 |
| 2 | Kiingereza | Saa 4 dakika 40 | 7 | Saa 4 dakika 40 | 6 |
| 3 | Hisabati | Saa 4 | 6 | Saa 3 dakika 20 | 5 |
| 4 | Sayansi na Teknolojia | Saa 3 dakika 20 | 5 | Saa 3 dakika 20 | 5 |
| 5 | Maarifa ya Jamii | Saa 2 | 3 | Saa 2 | 3 |
| 6 | Uraia na Maadili | Saa 3 dakika 20 | 5 | Saa 3 dakika 20 | 5 |
| 7 | Stadi za Kazi | -- | - | 1: 20 | 2 |
| 8 | Dini | Dakika 40 | 1 | Dakika 40 | 1 |
| | **Jumla ya muda wa kujifunza na idadi ya vipindi** | **Saa 21 Dakika 20** | **32** | **Saa 21 Dakika 20** | **32** |
| **Masomo ya kuchagua** | | | | | |
| 9 | Kifaransa/Kiarabu | Saa 1 Dakika 20 | 2 | Saa 1 Dakika 20 | 2 |
| | **Jumla ya muda wa kujifunza na idadi ya vipindi** | **Saa 1 Dakika 20** | **2** | **Saa 1 Dakika 20** | **2** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Shughuli katika mtaala wa ziada** | | | | | |
| 10 | Klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza | Saa 1 Dakika 20 | 2 | Saa 1 Dakika 20 | 2 |
| 11 | Elimu ya michezo na sanaa | Saa 1 Dakika 20 | 2 | Saa 1 Dakika 20 | 2 |
| 12 | Uzalishaji mali | Dakika 40 | 1 | Dakika 40 | 1 |
| 13 | Kujisomea/maktaba | Dakika 40 | 1 | Dakika 40 | 1 |
| | **Jumla ya muda wa kujifunza** | Saa 4 | **6** | Saa 4 | **6** |
| | **Jumla ya muda wa kusoma na idadi ya vipindi katika wiki** | **Saa 25 Dakika 20** | **38** | **Saa 25 Dakika 20** | **38** |

# Kujifunza Somo la Elimu ya Dini

## 10.1 Utangulizi

Mtaala wa Elimu ya Msingi umezingatia mahitaji ya Somo la Elimu ya Dini. Wanafunzi watajifunza Somo la Elimu ya Dini siku yoyote itakayopendekezwa na shule husika isipokuwa siku ya Ijumaa.

## 10.2 Siku za Kujifunza Somo la Elimu ya Dini

Siku ya Ijumaa masomo yatafundishwa hadi saa 6 mchana. Kuanzia saa 6 hadi saa 8 mchana hakutakuwa na vipindi vitakavyofundishwa kwa shule zote na kwa wanafunzi wote. Hii ni kwa sababu inatolewa nafasi kwa wanafunzi wa madhehebu yanayoabudu siku ya Ijumaa kushiriki ibada. Wanafunzi wasioshiriki katika ibada ya jumaa watumie muda huo kujisomea wenyewe. Aidha wanaweza kushiriki katika shughuli nyingine zitakazopangwa na shule mpaka muda wa kumaliza masomo.

# Ufundishaji na Ujifunzaji

## 11.1 Utangulizi

Mtaala wa Elimu ya Msingi umezingatia nadharia ya kujifunza ambayo inasisitiza mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji. Kutokana na nadharia hii jukumu la mwalimu ni kumwezesha mwanafunzi kujifunza. Kila mwanafunzi ana uwezo wa kujifunza kwa kiasi fulani hadi hapo anapohitaji msaada wa mwalimu ili ajifunze zaidi. Mtaala huu unasisitiza matumizi ya mbinu shirikishi katika utekelezaji wake. Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika mbinu shirikishi humpa mwalimu fursa za kutenda na kushirikisha wanafunzi wote bila kujali tofauti zao. Mtazamo huu wa kufundisha na kujifunza umejikita katika falsafa ya Elimu ya Kujitegemea.

## 11.2 Madarasa Jumuishi na Madarasa Maalum

Serikali inaweka mkazo katika kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote wa Tanzania kupitia elimu jumuishi. Aina hii ya elimu inatambua kuwa kila mwanafunzi anaweza kujifunza na kufanikiwa. Mtaala huu unabainisha mambo ya kuzingatia katika kuhama kutoka katika madarasa ya kawaida kuelekea katika madarasa jumuishi na madarasa maalum. Mambo hayo ni kama yalivyofafanuliwa katika Jedwali Na. 19.

**Jedwali Na. 19: Ufundishaji na Ujifunzaji katika madarasa jumuishi na madarasa maalum**

| Mambo ya kuzingatia | Madarasa jumuishi | Madarasa maalum/vitengo |
|---|---|---|
| Idadi ya kazi za kutenda mwanafunzi | Idadi ya shughuli za kutenda mwanafunzi ziwe za kutosha kulingana na uwezo wake. Hata hivyo, kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum shughuli za kutenda zipunguzwe kulingana na uwezo na mahitaji maalum aliyonayo | Idadi ya shughuli za kutenda mwanafunzi ziendane na mfumo wa utoaji mafunzo katika Darasa lake |

| Mambo ya kuzingatia | Madarasa jumuishi | Madarasa maalum/vitengo |
|---|---|---|
| Muda wa kujifunza | • Muda wa kujifunza na kujibu maswali ya upimaji uwe ule uliokubalika katika mtaala wa wanafunzi wa kawaida. Hata hivyo, kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum muda uongezwe kulingana na mahitaji maalum na uwezo alionao<br>• Muda wa kujibu maswali ya upimaji darasani kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum uongezwe<br>• Muda wa kumaliza mafunzo katika ngazi moja kwenda nyingine uongezwe kulingana na mahitaji maalum na uwezo wa mwanafunzi anayehusika | • Muda wa kutenda shughuli mbalimbali za kujifunza kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum uongezwe kulingana na mahitaji maalum na uwezo wa mwanafunzi anayehusika<br>• Muda wa kujibu maswali ya upimaji darasani kwa mwanafunzi mlemavu uongezwe kulingana na mahitaji maalum na uwezo wa mwanafunzi anayehusika<br>• Muda wa kumaliza mafunzo katika ngazi moja kabla ya kwenda ngazi nyingine uongezwe kulingana mahitaji maalum na uwezo wa mwanafunzi anayehusika |

| Mambo ya kuzingatia | Madarasa jumuishi | Madarasa maalum/vitengo |
|---|---|---|
| | | • Muda wa kujifunza na kujibu maswali ya upimaji utaendana na mfumo wa utoaji wa mafunzo katika madarasa yao |
| Kiwango cha kutoa msaada katika kujifunza | Kila mwanafunzi apewe msaada kulingana na mahitaji yake. Vilevile kiwango cha utoaji msaada kwa mwanafunzi mlemavu aliyejumuishwa kiongezeke kulingana na mahitaji yake | Kiwango cha msaada unaotolewa kwa mwanafunzi kiongezeke kulingana na mahitaji yake |
| Vifaa na njia/mbinu za kufundishia na kujifunzia | • Vifaa na vielelezo vya aina mbalimbali vya kuona, kusikia na kugusa vitumike katika kujifunza kulingana na uwezo na mahitaji maalum aliyonayo<br>• Mbinu mbalimbali shirikishi za kufundishia na kujifunzia zitumike kulingana na uwezo wa mwanafunzi na kulingana na mahitaji maalum aliyonayo<br>• Kuwepo na mpango wa mwanafunzi mmojammoja kufundishwa na kujifunza kulingana na kiwango cha mahitaji maalum yake | • Vifaa na vielelezo vya aina mbalimbali vya kuona, kusikia na kugusa vitumike katika kujifunza kulingana na mahitaji maalum aliyonayo<br>• Mbinu mbalimbali shirikishi za kufundishia na kujifunzia zitumike kulingana na mahitaji maalum ya kila mwanafunzi |

| Mambo ya kuzingatia | Madarasa jumuishi | Madarasa maalum/vitengo |
|---|---|---|
| | | • Kuwepo na mpango wa mwanafunzi mmojammoja kufundishwa na kujifunza kulingana na kiwango cha mahitaji maalum yake |
| Ushiriki wa mwanafunzi katika kujifunza | Kila mwanafunzi ashiriki katika kujifunza. Mwanafunzi mwenye mahitaji maalum ashiriki kwa kiwango ambacho anaweza kushughulika kulingana na mahitaji maalum aliyonayo | Mwanafunzi mwenye mahitaji maalum ashiriki kwa kiwango ambacho anaweza kulingana na mahitaji maalum aliyonayo |
| Utatuzi wa matatizo ya kujifunza | Mwanafunzi afuate kanuni zilizowekwa katika utatuzi wa matatizo wakati wa kujifunza na kutenda shughuli mbalimbali. Hata hivyo, mwanafunzi mwenye mahitaji maalum abadilishiwe kanuni zilizowekwa katika utatuzi wa matatizo hususani yale magumu, kulingana na kiwango cha mahitaji maalum aliyonayo | Mwanafunzi abadilishiwe kanuni zilizowekwa katika utatuzi wa tatizo, hususani yale magumu, kulingana na kiwango cha mahitaji maalum yake |

| Mambo ya kuzingatia | Madarasa jumuishi | Madarasa maalum/vitengo |
|---|---|---|
| Matarajio katika kujifunza | Matarajio yaliyopangwa/ yanayotegemewa yahimizwe. Hata hivyo, kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum matarajio mbadala yapangwe/ yakusudiwe | Matarajio mbadala yapangwe/yakusudiwe kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum |
| Namna ya kupata mrejesho wa kujifunza | Mwanafunzi asiye na mahitaji maalum arejee alichojifunza kwa njia iliyobainishwa. Mwanafunzi mwenye mahitaji maalum abadilishiwe namna ya kurejea alichojifunza kulingana na uwezo wake | Mwanafunzi mwenye mahitaji maalum abadilishiwe namna ya kurejesha alichojifunza kulingana na mahitaji maalum na uwezo wake |
| Uchaguzi wa Umahiri | Mwanafunzi ajifunze kilichoelekezwa. Hata hivyo, yule mwenye mahitaji maalum abadilishiwe kinachofundishwa kulingana na mahitaji maalum aliyonayo na uwezo wake | Mwanafunzi mwenye mahitaji maalum abadilishiwe kinachofundishwa kulingana na mahitaji maalum na uwezo wake |
| Lugha | Lugha ya kawaida itumike kwa mwanafunzi asiye na mahitaji maalum. Lugha sahihi ya kufundishia itumike kulingana na aina ya mahitaji maalum aliyonayo mwanafunzi (mfano, Lugha ya alama kwa mwanafunzi kiziwi | Lugha sahihi ya kufundishia itumike kulingana na aina ya mahitaji maalum aliyo nayo mwanafunzi (mfano, Lugha ya alama kwa mwanafunzi kiziwi |

| Mambo ya kuzingatia | Madarasa jumuishi | Madarasa maalum/vitengo |
|---|---|---|
| Ukaaji wa darasani | Ukaaji wa darasani uwe wa kawaida unaozingatia kila mwanafunzi kujifunza bila kikwazo. Ila kwa wale wenye mahitaji maalum ukaaji uzingatie aina ya mahitaji maalum aliyonayo na ushiriki wake katika kujifunza na wenzake wasio na mahitaji maalum | Ukaaji wa darasani kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalum uzingatie aina ya mahitaji maalum aliyonayo na ushiriki wake katika kujifunza |
| Usalama | Usalama wa kila mwanafunzi uzingatiwe, hususani ule wa mwenye mahitaji maalum kama ulemavu ngozi | Usalama wa kila mwanafunzi uzingatiwe kulingana na hali ya mahitaji maalum aliyonayo. |

## 11.3 Shughuli katika Mtaala wa Ziada

Shughuli katika Mtaala wa Ziada zitafanyika kwa lengo la kuimarisha maarifa na stadi ambazo mwanafunzi amejifunza ndani ya darasa. Hii itamwezesha mwanafunzi kuchangamana na wanafunzi wengine pamoja na mazingira ya nje ya darasa. Muktadha huu huimarisha ujenzi wa maana kwa yale anayojifunza. Shughuli hizo zitajumuisha klabu za masomo na maeneo mengine ya kujifunza. Vilevile zitakuwepo shughuli za michezo, uzalishaji mali, utamaduni, malezi na unasihi. Shughuli hizi zitawezesha wanafunzi kujifunza kwa kina. Ufuatao ni ufafanuzi wa shughuli katika Mtaala wa Ziada:

**a) Klabu za masomo**

Klabu hizi zitahusisha masomo mbalimbali na klabu za masuala mtambuka. Hizi ni kama klabu ya mazingira, VVU na UKIMWI, jinsia na haki za mtoto. Nyingine ni kama klabu ya stadi za maisha, kupinga/kudhibiti rushwa, afya, uelimishaji rika, biashara na usalama barabarani.

b) **Michezo na sanaa**

Wanafunzi watahimizwa kucheza michezo mbalimbali ili kuibua vipaji na vipawa ambavyo vitapaswa kuendelezwa. Michezo itafanyika kwa wanafunzi wote kufuatana na ratiba itakayopangwa na shule husika. Michezo hiyo ni pamoja na: uigizaji, uimbaji na riadha. Mingine ni kama mpira wa miguu, mikono, kikapu, wavu, meza, mchezo wa bao. Umahiri katika shughuli za michezo umegawanywa kimadarasa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 20.

**Jedwali Na. 20 Umahiri katika shughuli za michezo na sanaa kwa Darasa la III-VII**

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1. Kujenga stadi za ukakamavu kwa kushiriki katika michezo mbalimbali | 1.1 Kujenga mwili wenye nguvu kwa kushiriki michezo mbalimbali<br>1.2 Kujenga misuli stahimilivu kwa kushiriki michezo na sanaa<br>1.3 Kujenga kasi ya utendaji wa mwili kwa kushiriki michezo na sanaa<br>1.4 Kuwa na wepesi wa kufikiri na kufanya uamuzi sahihi kwa kucheza michezo anwai |
| 2. Kucheza michezo na kutenda kazi za sanaa kwa ustadi | 2.1 Kuwa na hali ya ushindani katika michezo na sanaa<br>2.2 Kuwa mbunifu katika kucheza na kutenda kazi za sanaa<br>2.3 Kutumia stadi mbalimbali za michezo na sanaa katika kuleta burudani |

c) **Uzalishaji mali**

Wanafunzi watafanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali shuleni. Madhumuni yake ni kuongeza kipato na kukuza stadi zao za ujasiliamali. Shughuli hizo ni kama kuendesha duka la shule na kulima busatni za mboga na maua.

Vilevile watafanya shughuli ya ufugaji, kilimo, ufinyanzi, ususi, uchongaji, uchoraji na biashara ndogondogo. Aidha watahimizwa kubuni vitega uchumi vya shule.

**d) Burudani**

Burudani ni shughuli anazofanya mtoto kujiburudisha mwili na akili awapo shuleni. Shughuli anwai zikiwamo ziara na matamasha zitafanyika mara moja kwa muhula. Kila shule itaainisha na kupanga shughuli za burudani zitakazoshirikisha wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalum. Hii itakuza usawa na ushirikiano miongoni mwa wanafunzi. Tuzo zitatolewa kwa wanafunzi watakaofanya vizuri ili kuwamotisha kuendeleza vipaji vyao. Mtaala huu umelenga kufikia mafanikio yafuatayo kutokana na kuendeleza burudani shuleni:

(i) kuibua vipaji na ubunifu wa wanafunzi;

(ii) kuendeleza vipaji binafsi vya wanafunzi kama vile kuigiza, kucheza dansi, kuimba, kucheza michezo pamoja na kubuni na kutengeneza vitu mbalimbali;

(iii) kuwezesha wanafunzi kuburudisha akili na miili yao;

(iv) kuwezesha wanafunzi kujifunza mambo mbalimbali kwa vitendo; na

(v) kukuza ari binafsi ya wanafunzi kupenda kusoma masomo mengine ya taaluma. Walimu na wanafunzi wenye mwelekeo katika fani mbalimbali watasaidiana na wataalamu katika usimamizi wa shughuli za burudani shuleni.

# Rasilimali katika Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi

## 12.1 Utangulizi

Viwango vya rasilimali katika utekelezaji wa mtaala vimegawanywa katika makundi makuu manne. Makundi hayo ni rasilimali watu, vitu, muda na fedha.

## 12.2 Rasilimali Watu

Rasilimali watu ni nguzo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa mtaala, hususani shughuli za kufundisha na kujifunza shuleni. Rasilimali watu inajumuisha mwalimu mahiri

Mwalimu bora katika Elimu ya Msingi awe amepata mafunzo ya kufundisha ngazi hii katika chuo kinachotambuliwa na serikali. Sifa za mwalimu katika Elimu ya Msingi zimefafanuliwa kwenye kiunzi cha umahiri wa mwalimu. Sifa kuu za mwalimu wa ngazi hii ni kuwa mahiri katika kufundisha, kupima na kufanya tathmini. Sifa hizo zinafafanuliwa hapa chini:

### 12.2.1 Kufundisha

Mwalimu mahiri anapaswa kuandaa na kufundisha somo linalomwezesha mwanafunzi kukuza umahiri wake katika nyanja mbalimbali. Mwalimu huyo ataonesha uwezo wa:

a) kutayarisha wanafunzi wanafunzi katika kujifunza KKK;
b) kuhusianisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu;
c) kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia stadi mbalimbali.
d) kuhusianisha stadi mbalimbali na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji;
e) kufundisha wanafunzi wenye uwezo tofauti;
f) kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika kufundisha;
g) kuandaa azimio la kazi na andalio la somo analofundishia;

h) kutumia kwa usahihi njia/mbinu zinazoshirikisha mwanafunzi katika kujifunza; na
i) kutoa mrejesho kwa mwanafunzi na wazazi utakaoboresha ujifunzaji.

### 12.2.2 Kupima ujifunzaji wa mwanafunzi na kufanya tathmini

Mwalimu mahiri ataonesha maarifa na stadi za kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi wake. Hivyo ataweza:-

a) kuandaa zana zinazofaa kumpima mwanafunzi katika ujifunzaji kwa kila umahiri;
b) kutumia njia zinazofaa kumpima mwanafunzi katika kila umahiri;
c) kutunza kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji wa kila umahiri;
d) kutumia matokeo ya upimaji na tathmini kuboresha ufundishaji wake na ujifunzaji wa wanafunzi; na
e) kutoa mrejesho kwa mwanafunzi na wazazi ambao utaboresha ufundishaji na ujifunzaji.

## 12.3 Rasilimali Vitu

Rasilimali vitu inahusisha vifaa mbalimbali vitakavyosaidia utekelezaji wa mtaala. Rasilimali vitu inajumuisha:

### 12.3.1 Vifaa vya kufundishia na kujifunzia

Vifaa ya kufundishia na kujifunzia ni muhimu katika utekelezaji wa mtaala. Vifaa hivyo ni pamoja na kivunge cha kujifunzia stadi za KKK na vifaa saidizi ambavyo vinafafanuliwa hapa chini:

**a) Kivunge cha kujifunzia stadi za KKK**

Darasa la I na la II watatumia kivunge chenye vifaa vya kujifunzia na kufundishia stadi za KKK. Kivunge hicho kimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya WyEST. Kivunge kitakuwa na chati za namba, maneno, herufi na chati za mwili wa binadamu. Vilevile kitakuwa na kadi za namba na herufi kwa idadi iliyoainishwa kwa darasa husika.

b) **Vifaa vya mtaala**

Mihtasari, miongozo, vitabu na zana za kufundishia na kujifunzia ni baadhi ya vifaa muhimu vya mtaala. Vifaa hivi huwezesha kufikiwa kwa malengo ya utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi. Vitabu vya kiada vitakavyotumika ni vile vilivyoidhinishwa na WyEST. Mihtasari na miongozo ya masomo itakayotumika ni ile iliyoandaliwa na TET na kuidhinishwa na WyEST. Kufundisha na kujifunza kutafanikiwa ikiwa vifaa vya sayansi na TEHAMA vitakuwepo shuleni na kutumiwa kwa usahihi. Mifano ya vifaa hivyo ni vifani, vinasa sauti (CD na DVD) na kompyuta. Aidha, kila shule inatakiwa kuwa na vifaa na vitendea kazi vya michezo, sanaa na fani mbalimbali.

c) **Vitabu vya ziada**

Wadau mbalimbali wa elimu wataandaa vitabu vya ziada.TET itavifanyia tathmini kwa kuzingatia vigezo na mahitaji ya Mtaala wa Elimu ya Msingi. WyEST itathibitisha matumizi ya vitabu tajwa shuleni.

d) **Vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum**

Vifaa saidizi kama vile vya kuona, kusikia na kugusa vitumiwe katika kujifunza kulingana na mahitaji maalum aliyonayo mwanafunzi. Mifano ya vifaa hivyo ni mashine za breli, vitabu vya sauti, vikuza sauti na vikuza maandishi kwa wenye uoni hafifu.

### 12.3.2 Samani na majengo

Samani na majengo yazingatie wanafunzi wa aina zote wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalum. Samani na majengo kwa ajili ya wanafunzi wa Darasa la I-II yazingatie umri na mahitaji yao katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa Darasa la III-VII vitazingatia mwongozo uliowekwa na WyEST. Kwa mfano, zifuatazo ni sifa za chumba cha darasa na kona za kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wa Darasa la I-II:

a) **Chumba cha darasa**

Chumba cha darasa kinatakiwa kuzingatia yafuatayo:

(i) ukubwa wa kila chumba cha darasa usipungue upana mita 6.0 na urefu mita 8.0;

(ii) ndani ya chumba cha darasa wanafunzi wasizidi 45;

(iii) dawati moja liwe kwa wanafunzi wawili;

(iv) nafasi kati ya dawati na dawati iwe mita 1.0;

(v) matumizi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(vi) pawepo kiti na meza kwa ajili ya mwalimu na msaidizi wake;

(vii) pawepo kabati au/na shelfu kwa ajili ya kuhifadhi vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

(viii) pawepo ubao mmoja (1) wa kuandika wenye ukubwa wa mita 1.2 upana na urefu mita 3.0 na ubao wa kutundika zana za kufundishia wenye ukubwa wa mita 1.2 upana na urefu mita 2.4; na

(ix) pawepo vibao vidogo vya kujifunzia kuandika kwenye kona tatu za chumba kwa ajili ya mazoezi ya wanafunzi.

b) **Kona za kujifunzia**

Kila chumba cha darasa kitakuwa na kona ya kusomea/kijifunzia yenye sifa zifuatazo:

(i) iwe na shelfu, vitabu vya kujisomea na kadi mbalimbali za kusoma;

(ii) iwe na viti, meza, benchi au mikeka; na

(iii) iwe na vifaa vya watoto wenye mahitaji maalum kama vile vitabu vya sauti na vinasa sauti.

## 12.3.3 Viwanja vya michezo

Maeneo ya michezo yenye ukubwa wa kutosha yatakuwepo shuleni. Kila eneo litazingatia mahitaji ya wanafunzi wote. Aidha, maeneo haya yasiwe na vitu vinavyoweza kudhuru wanafunzi.

## 12.4 Rasilimali Muda

Muda wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi ni miaka saba. Kila mwanafunzi atapaswa kujifunza kwa wiki 268 sawa na siku 1334 kwa mwaka kwa miaka saba. Muda huu utatumika ili kufikia umahiri uliokusudiwa.

## 12.5 Rasilimali Fedha

Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi utategemea uchangiaji wa fedha na mali kutoka kwa wadau mbalimbali. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi pamoja na wabia wa maendeleo ya elimu wanategemewa kuweka nguvu yao pamoja katika kuhahakisha elimu bora inatolewa nchini.

# Upimaji wa Maendeleo ya Mwanafunzi

## 13.1 Utangulizi

Upimaji ni sehemu muhimu katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji. Kupima kutamwezesha mwalimu kubaini kufikiwa kwa ujenzi wa umahiri uliokusudiwa. Kupima kutafanyika kwa kutumia zana mbalimbali zikiwemo mitihani ya kuandika, uchunguzi makini, mahojiano, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi na orodha hakiki. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi utahusisha upimaji wa: awali, endelevu, gunduzi, chekeche na upimaji tamati. Upimaji endelevu utatoa mrejesho kwa mwalimu na mwanafunzi ili kuboresha ujifunzaji na ufundishaji. Upimaji tamati utahusisha pia upimaji wa kitaifa ambao utafanyika kwa Darasa la II, IV na la VII. Yafuatayo ni maelezo kuhusu upimaji utakaofanywa kwa mwanafunzi.

## 13.2 Upimaji wa Awali

Upimaji wa awali utafanyika kabla ya mafunzo ili kupima kiwango cha uelewa na umahiri alionao mwanafunzi kabla ya mafunzo rasmi. Upimaji huu utafanywa mara tu mwanafunzi anapofika shuleni. Lengo lake ni kumwezesha mwalimu kutambua mahitaji binafsi ya mwanafunzi. Mahitaji hayo atayatumia kuandaa mipango ya kuwawezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa. Upimaji huu pia unaweza kutumika katika kuwapanga wanafunzi katika makundi kwa kuzingatia mahitaji yao. Shule zinatakiwa ziwe na utaratibu wa kuwapima wanafunzi kabla ya kuanza masomo ya Darasa la I.

## 13.3 Upimaji Gunduzi na Majaribio Chekeche

Upimaji huu ni sehemu ya upimaji endelevu. Utafanyika ili kupata taarifa kuhusu uwezo wa mwanafunzi katika kumudu stadi mbalimbali. Taarifa za upimaji zitatumika kutoa ushauri na msaada stahiki kwa wanafunzi wenye vikwazo mahsusi katika kujifunza. Wakati fulani msaada wa mtaalamu wa afya unaweza kuhitajika hasa kwa watoto wenye mahitaji maalum.

Pamoja na upimaji gunduzi, majaribio chekeche au mitihani chekeche itatumika. Lengo lake ni kuwabaini wanafunzi wenye vikwazo katika kujifunza stadi mbalimbali ili kuandaa mipango ya kuwasaidia. Aina hii ya upimaji inaweza kufanyika baada ya wanafunzi kujifunza kwa miezi mitatu na kuendelea. Yapo majaribio na mitihani chekeche ambayo imeandaliwa kutokana na tafiti mbalimbali ambayo inaweza kutumika. Aidha, upimaji gunduzi utahusisha mtihani wa kuandika, maswali ya ana kwa ana na uchunguzi makini ulioandaliwa na walimu shuleni. Lengo ni kuwabaini wanafunzi wenye vikwazo ili kuandaa mipango ya kuwawezesha katika kujifunza. Hata hivyo kutakuwepo na mtihani wa taifa wa Darasa la II na IV wenye lengo hilohilo.

## 13.4 Upimaji Endelevu

Upimaji huu utafanyika wakati wote wa ufundishaji na ujifunzaji ili kutoa mrejesho kwa mwalimu na mwanafunzi. Mrejesho utamwezesha mwalimu kuelewa maeneo yenye changamoto ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo. Kwa mfano, mwalimu atautumia kubaini mwanafunzi mwenye matatizo ya ujifunzaji ili aweze kusaidiwa. Zana za upimaji zitakazotumika ni pamoja na uchunguzi makini, mahojiano, mazoezi, maswali ya ana kwa ana, mkoba wa kazi na mtihani wa kuandika. Upimaji huu pia, utatumika kubaini vipaji mbalimali vya mwanafunzi kama ubunifu, uchoraji, sanaa na michezo. Aidha, utahusisha pia mitihani ya mwisho ya mihula ambayo italenga kubaini uwezo wa mwanafunzi katika stadi mbalimbali.

## 13.5 Upimaji Tamati

Upimaji huu utafanyika mwisho wa kila mwezi na muhula. Mtihani wa mwisho utatumika kama kigezo cha wanafunzi kutoka ngazi moja kwenda nyingine. Upimaji huu utahusisha mtihani wa kuandika, maswali ya ana kwa ana na uchunguzi makini.

## 13.6 Upimaji wa Kitaifa

Kutakuwa na upimaji wa kitaifa mwisho wa Darasa la II, IV na VII.

Upimaji huu utaandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania na ratiba yake itakuwa moja kwa nchi nzima. Baraza la Mitihani la Tanzania litatoa matokeo ya upimaji ya nchi nzima na yatatumika katika shule husika ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ufuatiliaji wa usimamizi na usahihishaji utafanywa na maofisa wa Baraza la Mitihani la Tanzania pamoja na maofisa kutoka maeneo mengine yanayohusika na usimamizi wa Elimu ya Msingi. Yafuatayo ni maelezo kuhusu upimaji wa kitaifa wa mwisho wa Darasa la II, IV na VII.

**a) Upimaji wa Darasa la II**

Upimaji wa kitaifa mwisho wa Darasa la II utakuwa na lengo la jumla la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo upimaji huu hautakuwa wa mchujo bali utatumika kubaini kiwango cha utendaji wa mwanafunzi kulingana na umahiri uliokusudiwa. Matokeo ya upimaji huu yatatumika kuandaa mpango wa kuwasaidia wanafunzi watakao bainika kuwa na vikwazo katika kujifunza pamoja na wale wenye mahitaji maalum. Zana mbalimbali za upimaji zitakazotumika ni kama maswali ya kuandika, kusoma na hojaji. Vigezo vitakavyozingatiwa katika upimaji huu vimeelezwa hapa chini:

**(i) Upimaji wa umahiri katika kusoma**

Mwanafunzi wa Darasa la II anatarajiwa kutenda yafuatayo:

- kutambua na kutamka sauti za herufi atakazopewa;
- kusoma kwa usahihi na ufasaha maneno 50 kwa dakika;
- kusoma kwa usahihi maneno yasiyo na maana 40 kwa dakika;
- kusoma kwa ufahamu kifungu cha habari na kutoa majibu sahihi;na
- kusoma msamiati unaolingana na ngazi ya darasa lake.

(ii) **Upimaji wa umahiri katika kuandika**

Mwanafunzi wa Darasa la II anatarajiwa kutenda yafuatayo:

- kuandika maneno na sentensi sahili kwa usahihi;
- kutumia herufi kubwa na ndogo kwa usahihi;
- kutumia alama za uandishi kwa usahihi (nukta, mkato, alama ya mshangao na alama ya kiulizo); na
- kuandika hadithi fupi au aya yenye ushikamani, tahajia, muundo wa sentensi na vituo sahihi.

(iii) **Upimaji wa umahiri katika kuhesabu**

Mwanafunzi wa Darasa la II anatarajiwa kutenda yafuatayo:

- kujumlisha na kutoa kwa namba zenye tarakimu tatu;
- kukamilisha mtiririko wa namba kwa kujaza namba moja inayokosekana kwenye mtiririko wa namba nne;
- kubaini na kuhusianisha michoro inayoonesha sehemu za michoro na sehemu za numerali;
- kubaini na kuchora maumbo rahisi na mistari;
- kutumia vipimio rahisi ambavyo ni rasmi na visivyo rasmi
- kutambua muda, ujazo, uzito na urefu; na
- kutafsiri data rahisi zinazoelezea vitu au shughuli.

b) **Upimaji wa Darasa la IV na la VII**

Upimaji wa kitaifa kwa Darasa la IV na VII utatumika kubaini kama mwanafunzi amefikia umahiri unaotarajiwa ili avuke ngazi moja kwenda ngazi nyingine (yaani kutoka Darasa la IV kwenda la V au kutoka Darasa la VII kwenda Kidato cha Kwanza). Mtihani wa Darasa la IV hautakuwa wa mchujo, bali utatumika kubaini upungufu wa ujifunzaji alionao mwanafunzi ili asaidiwe kabla hajaingia ngazi ya juu. Upimaji wa Darasa la IV utahusisha mtihani wa kuandika, maswali ya ana kwa ana na uchunguzi makini.

# Usimamizi wa Mtaala

## 14.1 Utangulizi

Usimamizi wa mitaala ni jambo muhimu katika kuhakikisha inatelekezwa kama ilivyokusudiwa. Usimamizi wa utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Msingi utafanyika kuanzia ngazi ya shule hadi Wizara. Vilevile, usimamizi utaenda sambamba na utoaji wa mafunzo endelevu kwa watekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mtaala husika.

## 14.2 Majukumu ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa

Usimamizi wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Msingi utafanyika kuanzia ngazi ya shule hadi Wizara. Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ndiyo msimamizi mkuu wa utekelezaji wa mtaala huu kupitia Idara ya Elimu. Usimamizi katika ngazi ya shule ni nguzo kuu katika utekelezaji wa mtaala. Walimu wakuu, kamati za shule na Maafisa Elimu Kata watakuwa ndio wasimamizi wakuu katika ngazi hii. Hivyo, kwa kupitia vikao watajadili maendeleo ya utekelezaji wa mtaala. Wakurugenzi wa manispaa au halmashauri kupitia maafisa elimu wa wilaya watasimamia mtaala katika ngazi ya wilaya. Pia, maafisa elimu wa mkioa watasimamia utekelezaji wa mtaala katika ngazi ya mikoa. Kwa ujumla katika usimamizi wa mtaala huu kutakuwa na ugatuaji wa baadhi ya majukumu ya elimu kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

## 14.3 Mafunzo Endelevu ya Mtaala kwa Watekelezaji

Walimu, wasimamizi, wathibiti ubora wa shule pamoja na wadau wengine wa Mtaala wa Elimu ya Msingi, watapatiwa mafunzo yatakayowawezesha kutekeleza mtaala huu kwa ufanisi. TET itandaa na kuendesha mafunzo haya ambayo yatatolewa kwa njia ya ana kwa ana na ya masafa. Vilevile vyuo vya ualimu na Vyuo Vikuu vinavyoandaa walimu wa ngazi hii ya elimu vitakuwa na jukumu la kufundisha walimu tarajali kuhusu mtaala huu.

## 14.4 Ufuatiliaji na Tathmini ya Mtaala wa Elimu ya Msingi

Ufuatiliaji na tathmini ya mtaala huu utafanyika kwa kuzingatia Miongozo ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini ya mtaala inayotolewa na WyEST na wizara ya OR - TAMISEMI.

### 14.4.1 Ufuatiliaji wa mtaala

Ufuatilaji wa utekelezaji wa mtaala unalenga kukusanya taarifa kuhusu ufanisi wa mtaala. Wadau wote wakuu wa Elimu watahusika katika kufuatilia utekelezaji wa mtaala wakiwemo wazazi, wajumbe wa kamati za shule, walimu, wanafunzi na wathibiti ubora. Wafuatiliaji hawa wamegawanyika katika makundi mawili: wafuatiliaji wa ndani na wa nje. Walimu wakuu ni wafuatiliaji wa ndani na wa mwanzo wa utekelezaji wa mtaala. Miongozo ya ufuatiliaji na tathmini ya mtaala ya wizara zitakazohusika na elimu itatoa maelezo ya majukumu ya kila mdau katika kuhakikisha mtaala unatekelezwa kwa ufanisi. Taarifa za ufuatiliaji zitachambuliwa na kupelekwa TET na kwa wadau wakuu wengine wa elimu ambapo zitatumika katika mikakati ya kuimarisha utekelezaji wa mtaala.

### 14.4.2 Tathmini ya mtaala

Tathmini ya mtaala huu italenga kubaini maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Tathmini huangalia mambo yote yaliyo katika mtaala. Mambo haya hujumuisha malengo na umahiri uliokusudiwa, maudhui na njia za kufundishia na kujifunzia. Mengine ni upatikanaji wa vifaa na zana za upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi, uwezo wa walimu katika kufundisha na mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Tathmini endelevu na tamati za mtaala zitafanyika kwa kuhusisha wadau mbalimbali wakiongozwa na TET. Tathmini endelevu itafanyika muda wote wa ufundishaji na ujifunzaji wakati tathmini tamati itafanyika kila mara baada ya kukamilika kwa mzunguko wa elimu ya msingi.

# Ujifunzaji na Viwango vya Upimaji Darasa la III- VII

## 15.1 Utangulizi

Mafanikio ya utekelezaji wa mtaala huu yatapimwa kwa kuangalia kiwango cha kutenda au umahiri anuwai wa kila mwanafunzi. Maelezo ya utaratibu wa upimaji husika yametolewa katika sehemu hii ya mtaala.

## 15.2 Vigezo na Viwango vya Kupima

Vigezo na viwango vya kupima utendaji wa mwanafunzi vitatolewa na wizara zinazohusika na elimu nchini. Kuhusu mtaala huu, vigezo na viwango hivyo vya utendaji vinatolewa kimasomo na kuainishwa katika Jedwali Na. 21.

**Jedwali Na. 21: Vigezo na viwango vya kupima utendaji wa mwanafunzi wa Darasa la III-VII**

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| Kiswahili | 1. Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika:<br>1. kubaini sauti katika matamshi ya silabi, maneno na herufi mwambatano;<br>2. kutumia lugha ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali; na<br>3. kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. |

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| | 2. Kuonesha uelewa wa jambo alilosikiliza au kulisoma | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika:<br>1. kusikiliza na kumudu mazungumzo; na<br>2. kusoma maandiko mbalimbali kwa ufasaha kwa kuzingatia kanuni za uandishi. |
| | 3. Kutumia msamiati katika miktadha mbalimbali | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika:<br>1. kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na hali mbalimbali;<br>2. kutumia maandishi katika kuandaa matini mbalimbali; na<br>3. kusoma na kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa kwenye matini mbalimbali. |
| Kiingereza | 1. Comprehend oral and written information | 1. The pupil will be assessed on his /her ability to comprehend information presented orally.<br>2. The pupil will be assessed on his /her ability to listen pronounce and read phonemic symbols. |

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| | 2. Communicate orally and through writing | The pupil will be assessed on his /her ability to communicate simple ideas through speaking and writing. |
| | 3. Use vocabulary through the four language skills (listening, speaking, reading and writing) | The pupil will be assessed on his/her ability to develop and use listening, speaking, reading and writing skills. |
| Hisabati | 1. Kutumia stadi mbalimbali katika maisha ya kila siku | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kutumia stadi za vipimo, maumbo na mafumbo katika miktadha mbalimbali. |
| | 2. Kutumia lugha ya kihisabati kutatua matatizo katika mazingira tofauti | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kutumia matendo ya namba na uhusiano wa namba na vitu kutatua matatizo katika miktadha mbalimbali. |
| | 3. Kutumia lugha ya kihisabati katika kuwasilisha wazo au hoja katika maisha ya kila siku | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kutumia dhana ya namba, takwimu na aljebra kuwasilisha wazo au hoja katika miktadha mbalimbali. |

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| Sayansi na Teknolojia | 1. Kufanya uchunguzi wa kisayansi na kiteknolojia katika maisha ya kila siku | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutumia nadharia za kisayansi na teknolojia kukuza matumizi ya stadi za uchunguzi katika mazingira yake. |
| | 2. Kutumia maarifa na stadi za kisayansi na kiteknolojia katika maisha ya kila siku | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutumia maarifa na stadi za kisayansi na kiteknolojia katika kutatua matatizo mbalimbali. |
| | 3. Kutumia maarifa na stadi za usafi wa mwili na utunzaji wa mazingira | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutumia kanuni za afya na kutunza mazingira katika maisha ya kila siku. |
| Maarifa ya Jamii | 1. Kutumia misingi ya uzalendo katika jamii | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika:<br>1. kujenga uhusiano mwema katika jamii;<br>2. kutumia utamaduni wake kwa usahihi katika miktadha mbalimbali; na<br>3. kutunza na kuenzi mashujaa wa Tanzania na Afrika kwa ujumla. |

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| | 2. Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika: 1.kutumia ramani, kuelezea sura ya nchi na maliasili zake pamoja na kugundua mabadiliko yanayoweza kutokea katika uso wa dunia kwa kutumia elimu ya mfumo wa jua. |
| | 3. Kufuata kanuni za kusimamia shughuli mbalimbali za kiuchumi katika jamii na taifa | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kubainisha shughuli za uzalishaji mali, kutumia stadi za ujasiriamali na kutumia kanuni kulinda rasilimali za nchi kwa maendeleo ya taifa. |
| | 4. Kuhakiki matukio na kuchukua tahadhari. | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kutunza kumbukumbu, mazingira na kupanga shughuli mbalimbali kulingana na hali ya hewa ya nchi yake. |
| Uraia na Maadili | 1. Kufuata taratibu za kuheshimu jamii | Mwanafunzi atapimwa kiwango cha uwezo wake wa kujipenda mwenyewe, kuwapenda watu wengine, kuipenda na kujivunia shule yake pamoja na kuipenda nchi yake kwa kuzienzi tunu za nchi na asili yake. |

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| | 2. Kufuata taratibu za kuthamini jamii. | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kujijali na kuwajali wengine, kutunza mazingira na vilivyomo na kujenga uhusiano mwema na watu wengine. |
| | 3. Kutumia misingi ya uwajibikaji | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kulinda rasilimali na maslahi ya nchi, kusimamia majukumu, kutii sheria na kanuni, kuonesha nidhamu binafsi na kuwa na ushirikiano na wenzake katika kutekeleza majukumu mbalimbali. |
| | 4. Kuonesha tabia ya kupenda kufikia malengo katika maisha | Mwanafunzi atapimwa kiwango chake cha kutumia kanuni katika maisha, kufikia malengo aliyojiwekea kwa kuwa na mtazamo chanya na kujifunza kwa kuchanganua mambo kiyakinifu. |
| | 5. Kutumia misingi ya uadilifu | Mwanafunzi atapimwa kiwango chake cha kuaminika katika jamii, kusimamia haki na kutimiza majukumu mbalimbali kwa uwazi na ukweli. |
| | 6. Kutumia misingi ya amani | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kuchangamana na watu wenye asili tofauti, kubaini tofauti za kiutamaduni na mitazamo katika jamii na kujenga urafiki na mataifa mengine. |

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| Kifaransa | 1. Comprendre à l'oral et à l'écrit des informations dans des situations de communication diverses | Des documents sonores et ecrits simples seront utilisés pour évaluer lapprenant. |
| | 2. S'exprimer à l'oral et à l'écrit dans des situations de communication diverses | L'expression orale et écrite de l'apprenant dans des situations diverses de communication. |
| | 3. Produire à l'oral et à l'écrit en utilisant le vocabulaire acquis dans des situations différentes | Des documents sonores et écrits simples seront utilisés pour évaluer le vocabulaire acquis par l'apprenant dans des situations diverses de communication. |

**Jedwali Na. 22a: Vigezo na Viwango vya kupima utendaji wa mwanafunzi wa Darasa la III-VII katika Somo la Kiarabu**

| تقويم الأداء | معايير التقويم | المادة |
|---|---|---|
| 1 يقوم التلميذ قدرته على فهم التعبيرات مشافهة.<br>2 يقوم التلميذ قدرته على إستماع ونطق وقراءة الحروف الهجائية وتمييز أصواتها. | معرفة وفهم الحروف نطقا وكتابة | اللغة العربية |
| يقوم التلميذ قدرته على التواصل بعبارات بسيطة من خلال الكلام والكتابة. | التواصل مشافهة ومن خلال الكتابة | |
| يقوم التلميذ قدرته على تنمية واستخدام المهارات اللغوية الأربعة. | اكتساب واستخدام المصطلحات اللغوية من خلال المهارات اللغوية الأربعة | |

**Jedwali Na. 22b: Tafsiri ya maneno ya Kiarabu katika Jedwali Na. 22a**

| Upimaji wa utendaji | Vigezo vya upimaji | Somo |
|---|---|---|
| Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika:<br>1. kuonesha uelewa wa sentensi mbalimbali kwa njia ya mazungumzo; na<br>2. kusikiliza, kutamka, kusoma herufi na kubaini sauti za herufi za Kiarabu. | 1. Kuonesha uelewa wa sentensi kwa kuzungumza na uelewa wa herufi kwa kutamka na kuandika | Kiarabu |
| Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kuwasiliana kwa kutumia sentensi mbalimbali kwa njia ya mazungumzo na maandishi. | 2. Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandishi | |
| Mwanafunzi atapimwa uwezo wake wa kukuza na kutumia umahiri wa stadi nne za lugha. | 3. Kutumia misamiati ya lugha kupitia umahiri wa stadi nne za lugha | |

Vigezo na viwango vya kupima utendaji vitakavyozingatiwa kwa shughuli katika Mtaala wa Ziada vimeainishwa katika Jedwali Na.22.

**Jedwali Na. 23: Vigezo na viwango vya kupima shughuli katika Mtaala wa Ziada**

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| Michezo na sanaa | 1. Kujenga stadi za ukakamavu kwa kushiriki katika michezo mbalimbali | Mwanafunzi atapimwa katika kushiriki michezo, kuwa mvumilivu na kufanya uamuzi katika shughuli za michezo na sanaa. |

| Somo | Vigezo vya upimaji | Upimaji wa utendaji |
|---|---|---|
| | 2.Kucheza michezo na kutenda kazi za sanaa kwa ustadi | Mwanafunzi atapimwa katika ushindani nidhamu, ushirikiano na uthubutu katika michezo na sanaa. |
| Klabu za masomo | 1. Kuunda klabu za masomo | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kuunda, kusimamia na kuongoza klabu za somo linalohusika. |
| | 2. Kushiriki shughuli za klabu za masomo | Mwanafunzi atapimwa katika kushiriki shughuli mbalimbali za klabu za masomo. |
| Uzalishaji mali | 1. Kubuni shughuli mbalimbali za kuzalisha mali | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kubuni na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kuzalisha mali shuleni na nyumbani. |
| | 2. Kutumia misingi ya shughuli za kuzalisha mali | Mwanafunzi atapimwa uwezo wake katika kusimamia shughuli za uzalishaji mali ili kuwa endelevu. |

# Marejeleo


Bajumuzi, J. (2002). *Performance of the Visually Impaired Pupils in Tanzania*. Dar es Salaam. (Unpublished Document).

Barnes, D. (1982). *Practical Curriculum Study*: Routledge and Kegan Paul: London.

East Africa Cummunity. (2013). *Draft Harmonised Curriculum Structures and Framework for East Africa Community.* Primary Education for East Africa.

Institute of Curriculum Development. (1990). *A summary Report on Baseline Survey on Primary, Secondary and Teacher Education Curriculum Reform in Tanzania Mainland*. Dar es Salaam. (Unpublished Document).

Ministry of Education and Culture. (1995). *Education and Training Policy.* Dar es Salaam

Ministry of Education and Culture. (2001). A *Baseline Survey on Knowledge, Attitudes and Practices (KAP) in Tanzania Mainland.* Dar es Salaam: UNFPA.

Ministry of Education and Culture. (2001). *Education Sector Development Plan: Primary Education Development Programme* (2002-2006), *Basic Education Development Committee (BEDC)*, July 2001 (Unpublished Document).

Ministry of Education and Culture. (2003). *Education Sector Development Plan: Primary Education Development Plan*: *Designs for the Improvement of Quality of Primary Education*. Dar es Salaam, April 2003: (Unpublished Document).

Morsh, C. J. (1977). *Planning Management and Ideology: Key Concepts for Undestanding Curriculum.* UK: Falmer Press.

Njabili, F. A. (1993). *Practical Guide for Classroom Measurement and Testing. The Basic Essentials.Dar es Salaam:* Mture Publishers.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (1999). *Ripoti ya Ufuatiliaji wa Muundo Mpya wa Masomo katika Shule za Msingi Tanzania Bara*. Dar es Salaam. (Andiko Lisilochapishwa).

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2003). *Ripoti ya Warsha ya Kudurusu Mada za Elimu Dhidi ya Ukimwi katika Masomo Chukuzi kwa Shule za Msingi na Sekondari.* TET, Dar Es Salaam.

Tanzania Institute of Education. (2004). *NCDF: A Guide to Innovative Teaching and Learning. Dar es Salaam.* (Unpulished Document).

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2004). *Ripoti ya Utafiti wa Kuboresha Mtaala wa Elimu ya Msingi*. Dar es Salaam (Kisawidi: Rekebisho la Kwanza): Agosti 2004.

Tanzania Institute of Education. (2004). *National Curriculum Development Framework (NCDF): Core Document.* Dar es Salaam. (Unpublished Document).

Tanzania Institute of Education. (2004). NCDF. *A Curriculum Guide to Primary Education. Dar es Salaam.* (Unpublished Document).

Tanzania Institute of Education. (2004). NCDF. *A Guide to Assessment and Examination*. Dar es Salaam, (Unpublished Document).

Tanzania Institute of Education. (2014). *Report of the Workshop for Curriculum Implementers and Supervisors on the Review of Pre-primary and Primary Curriculum* (unpublished Document).

Tanzania Institute of Education. (2014). *Report of the Workshop for Policy Makers and Curriculum Implementers on the Review of Pre-primary and Primary Curriculum* (unpublished Document).

Tanzania Institute of Education. (2014). *Report of the Workshop on Critical Analysis of Pre-primary and Primary Education Curriculum* (unpublished Document).

UNICEF. (2004). *Report on Baseline Survey on Gender. Sexuality. HIV/AIDS and Life Skills in Basic Education in Tanzania Mainland.* Dar es Salaam. (Unpublished Document).

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (1998). *Waraka wa Elimu Namba 5 wa Somo la Dini. Dar - es- Salaam:* WyEMU.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo. Dar-es-Salaam:* WyEMU.

Tanzania Institute of Education. (2019). *National Curriculum Framework for Basic and Teacher Education.* (unpublished Document).